# USIOGOPE MAJARIBU

## Ndipo Ukuu Wako Ulipo

**Ezekiel Vigello**

# USIOGOPE MAJARIBU

## Ndipo ukuu wako ulipo

---

Hatimiliki © April, 2018

EZEKIEL WILLIAM VIGELLO

MWANZA, TANZANIA

EAST AFRICA

Simu: +255 753 100 788

Barua pepe: zekbanger@gmail.com

Toleo la Kwanza: April, 2018

**ISBN: 978-9976-5270-6-3**

**Haki zote zimehifadhiwa**

---

Hakuna sehemu yoyote ya kitabu hiki inaruhusiwa kutolewa upya au kuhamishwa kwa namna au njia yoyote; kielektroniki au kiufundi au kwa kutoa nakala (photocopy), kurekodi kwa namna yoyote ya kuhifadhi habari au kurudishia tena bila idhini ya mwandishi kwa maandishi isipokuwa matumizi ya dondoo kwa lengo la kufundishwa au kujifunza.

*Kimepigwa chapa na: Gracious Printing Solution*

*Dar es salaam, Tanzania*

*Simu: +255 713 804 078*

# YALIYOMO

**UTANGULIZI**.......................................................................v
**SURA YA KWANZA** ........................................................1
**JITAMBUE ILI UWE HURU** ............................................1
**Ifahamu kweli**.....................................................................4
**Ijenge nafsi yako kwa Uthamani** ....................................8
**Boresha nafsi yako mara kwa mara**..............................11
**SURA YA PILI**..................................................................14
**SIRI KUU 5 KUHUSU MAJARIBU**................................14
**I. Jaribu ni Kawaida ya Wanadamu**.........................16
**II. Unaweza Kulimudu** ................................................18
**III. Mungu ni Mwaminifu**........................................21
**IV. Kuna Njia ya Kutokea**........................................24
**V. Lazima Upite Hapo ili Ukue**..................................27
**MAMBO YA KUFANYA UNAPOPITIA KWENYE JARIBU**.......................................................................30
**Endelea Kuwa na Fikra Njema** ....................................30
**Omba kwa Bidii**..........................................................33
**Amini Kwamba Utashinda**...........................................37
**Kaa Karibu na Watu Wanaokutia Moyo** .....................40
**Nani Anafaa Kukushauri?** .............................................42
**Usiogope**.......................................................................45
**SURA YA NNE** ..............................................................48
**USIPOTEZE MUDA** .......................................................48
**Usijiulize Itakuwaje** .......................................................49
**Fanya Jambo Mbadala**..................................................52


**Ishi Kama Hauna Changamoto** ....................................55
**Fikiria Maisha Bora Yajayo** ..........................................57
**Saidia Wengine Wanaopitia Changamoto**....................59
**SURA YA TANO** .................................................................63
**LIFANYE KOVU LAKO LIWE NA THAMANI**............63
**Weka Malengo Yako Kwa Upya**....................................64
**Fanya Jaribu Lako Kuwa Ushuhuda**............................67
**Kubali Kulipa Gharama**................................................70
**Kifanyie Kazi Ulichojifunza**..........................................72

Mpendwa Msomaji,

Mikononi mwako umeshika kitabu chenye thamani kubwa na kinachoweza kukufanya uwe mwenye furaha wakati wote, mshindi na mwenye mafanikio tele. Ezekiel Vigello ni mwandishi mahiri sana na vitabu vyake vimekuwa chachu ya maendeleo kwa watu wengi ndani na nje ya Tanzania. Kitabu chake cha kwanza kilichoitwa ‘The Paths of a Trader’ kilifanikiwa kutatuta changamoto nyingi za kimaisha na kutumika katika maamuzi ya kibiashara.

Nakuombea kwa Mungu kwamba usomapo kitabu hiki; upate uelewa na uweze kutendea kazi kile utakachojifunza kutoka kwenye maneno ya mwandishi huyu yaliyojaa hekima, ufahamu na maarifa yatokanayo na neno la Mungu aliye hai na anayekupenda! Kitabu hiki kifufue matumaini mapya na imani katika yeye atutiaye nguvu siku zote. Mungu akubariki sana na ninajua hakika ya kwamba baada ya kusoma kitabu hiki; maisha yako hayatakuwa kama ulivyo sasa! Amen.

Wako katika Kristo,



Emanuel Sylvester

Mkurugenzi Mtendaji

# UTANGULIZI

Maisha ya mwanadamu yamegawanyika katika nyakati mbalimbali muhimu ambazo humpasa kuzipitia ili mwanadamu awe bora zaidi. Endapo mwanadamu akikataa kupitia vipindi hivyo basi atadumaa. Kuna vipindi vya raha na vipindi vya changamoto. Vipindi vyote hivyo ni vya muhimu sana kwa mwanadamu; na ni kama vitamini imuwezeshayo mwanadamu kukua na kustawi.

Kuna mlolongo wa kimaisha ambao unapatikana katika Zaburi 23, nami nimeugawanya katika sehemu tatu yaani nyakati za utulivu, nyakati za misukosuko na nyakati za kupewa tunzo; ili tuweze kuona uhalisia wa maisha ya mwanadamu!

**Sehemu ya Kwanza (Utulivu);** neno la Mungu linasema "Bwana ndiye mchungaji wangu, Sitapungukiwa na kitu. Katika malisho ya majani mabichi hunilaza, Kando ya maji ya utulivu huniongoza. Hunihuisha nafsi yangu; na kuniongoza Katika njia za haki kwa ajili ya jina lake……."

Sehemu hii ya kwanza; Daudi anatuonesha ni kwa jinsi gani Mungu anatupenda wanadamu na

kutupa mambo yote yaliyo mema, yanayoleta utukufu mbele zake ili kutufanya tuwe wenye furaha na amani nyakati zote. Ni mpango wa Mungu kwamba tuyafurahie maisha na ndivyo tulivyo!

**Sehemu ya Pili (Misukosuko);** Neno la Mungu linasema, "……Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, Sitaogopa mabaya; Kwa maana Wewe upo pamoja nami, Gongo lako na fimbo yako vyanifariji……."

Sehemu hii ya pili; Daudi anatuonesha kwamba; japokuwa anazo neema nyingi kutoka kwa Bwana lakini bado anajua ya kwamba ni lazima atapita tu katika kipindi ambacho sio rafiki sana kwake. Lakini katika kipindi hicho kigumu bado anakiri kutokuogopa mabaya na kuamini kwamba Mungu yuko pamoja naye, pia anajua ya kwamba ni muhimu sana apitie changamoto ili aweze kustawi!

**Sehemu ya Tatu (Tunzo);** neno la Mungu linasema "……Waandaa meza mbele yangu, Machoni pa watesi wangu. Umenipaka mafuta kichwani pangu, Na kikombe changu kinafurika. Hakika wema na fadhili zitanifuata

Siku zote za maisha yangu; Nami nitakaa nyumbani mwa Bwana milele."

> Sehemu hii ya tatu; Daudi anatudhihirishia ya kwamba baada ya magumu ambayo mwanadamu huyapata ili aweze kuwa bora, Mungu humpa tunzo ya ushindi, humuinua juu ya watesi wake na kumstawisha zaidi.

Huu ndio mlolongo halisi wa kimaisha ya mwanadamu na haukwepeki, ukiukwepa hakika maisha yako hayatakuwa na mabadiliko. Karibu tuendelee kufunua siri nyingine nyingi zaidi!

## SURA YA KWANZA

## JITAMBUE ILI UWE HURU

Mungu alipomuumba mwanadamu alimuona kuwa ni kitu chema sana na cha kupendeza! Yaani ubunifu, busara na hekima ya Mungu iliyotumika kukuumba wewe ni ya hali ya juu sana kupita fahamu zote na uelewa wote wa mwanadamu!

> Natamani sana ungalijua kwamba Mungu anakuona wewe ni kitu chema na chenye thamani sana machoni pake! Hata kama ulizaliwa katika mazingira yanayotatanisha, fumbua macho yako na tambua ukweli halisi kuhusu wewe. Dunia hii inaweza kumfanya mwanadamu akasahau kuwa yeye ni nani kwa sababu ya changamoto na mapito yaliyomo ndani yake!

Nilikutana na rafiki mmoja akaniambia, “Kaka mimi sijui kama nitamaliza chuo” akainama kwa kunyong`onyea. Nikamuuliza “una tatizo gani linalokufanya kwa kinywa chako ukiri kuwa hautaweza kumaliza chuo?” akaniambia, “nimezaliwa kwenye familia ya kimasikini na wazazi wangu ni wazee sana halafu tumezaliwa watoto

wengi na wote hatuna mtu wa kutusaidia kutusomesha, hapa najitahidi kusoma kwa bidii lakini sina uhakika wa kupata pesa ya kulipa ada ya chuo.” Akaendelea, “wakati mwingine nikiwa najisomea usiku chumbani kwangu hua nafika wakati moyo unasita kuendelea kujisomea kwa sababu nasoma bila matumaini ya kumaliza chuo japokuwa nina uhakika wa kufaulu vizuri katika masomo yote!”

Niligundua kwamba kijana **amesahau yeye ni nani**!

> Usipojua uthamani ulionao na nguvu ya ajabu iliyomo ndani yako, ni rahisi sana wewe kuishi maisha yaliyo chini ya viwango ambavyo Mungu alivikusudia kwa ajili yako alipokuumba.

Ni jambo la kupendeza sana mwanadamu akipata maarifa yanayomfungua fahamu zake na kugundua ya kuwa yeye ni nani na ana uwezo gani ndani yake, pia ni vema kuupima au kuujaribu uwezo ulioko ndani yako kwa kufanya mambo yale ambayo haukuwahi kuyafanya hapo kabla kwa sababu ya hofu na kutokujua vema wewe ni nani na uwezo ulimo ndani yako ni upi!

Katika nchi zetu za kiafrika, kuna tamaduni mbalimbali zinazomfanya mwanadamu atambue kwa wakati husika yeye ni nani, uwezo alionao ni upi na majukumu

aliyonayo ni yapi! Kijana wa kiume asipopata malezi sahihi na mtu wa kumuongoza kuifumbua akili yake ili kutambua yanayompasa anaweza kubakia kuwa mvulana na sio mwanaume hata anapozeeka.

> Hivi unajua ya kwamba; Ndege aina ya Tai anaweza kuishi katikati ya Kuku na asiweze kuruka na kuona kuwa ni kawaida tu na pengine hata kujivunia hali hiyo ya kutokuruka endapo hatapewa taarifa sahihi kuhusu yeye ya kuwa yeye ana uwezo mkubwa kuliko wa kuku!

Uliishawahi kujiuliza kwa nini; watu wengi waliozaliwa na kuishi kijijini kwa muda mrefu huishia kufanya mambo yaleyale waliyoyakuta katika kijiji chao pasipo kufanya maboresho yoyote makubwa mpaka pale ambapo watatoka kwenda mjini na kugundua vitu bora zaidi ndipo wanahamishia ujuzi huo kwenye kijiji chao? Jibu ni jepesi, hawakujua kama wanaweza kufanya mambo hayo mazuri na ya kuvutia mpaka pale walipoona na kujiaminisha kuwa inawezekana kwani wanadamu wenzao wameweza kufanya tena kwa ustadi mkubwa sana.

## Ifahamu kweli

Unapoufahamu ukweli kuhusu wewe ndipo utagundua kuwa wewe ni kiumbe cha ajabu sana na chenye nguvu kubwa kuliko viumbe vingine. Nguvu aliyonayo mwanadamu haijalishi umbile lake lakini ni nguvu kubwa yenye uwezo wa kuibadili dunia na kufanya mambo yawe mazuri zaidi au mabaya zaidi. Hatuwezi kumlinganisha mwanadamu na tembo kwani mwanadamu anao utashi wakati tembo hana utashi japokuwa tembo analo umbile kubwa kuliko la mwanadamu!

> Watu wengi wamefungwa na mazingira yanayowazunguka na kuona hawawezi tena kufanya mabadiliko katika nyanja mbalimbali za maisha yao. Wakijiangalia maumbile yao, elimu zao, vipato vyao na mengineyo wanaona kwamba tayari wamefika mwisho hawana cha kufanya. Hakika ukifahamu nguvu iliyoko ndani yako hautakuwa mtu wa kawaida kawaida tu.

Mungu alikuuumba akakupumzia pumzi ya uhai na akaona ya kuwa amefanya kitu chema, sio bure! Umeumbwa kwa mfano wa Mungu ndugu sio mfano wa Ngedere au Nyani asiyekuwa na uwezo wa kufikiri na kuchukua maamuzi sahihi.

Tofauti iliyomo ndani yako na viumbe vingine ni kubwa sana. Usijidharau, usisikitike wala usijilaumu anza sasa kuitumia nguvu hiyo!

Mtoto anapozaliwa huwa hajui kama ana uwezo wa kuvuta kitu kwa mikono yake na kikasogea. Huanza kujifunza polepole tena kwa mazoezi na akishaona kuwa anaweza kushika vitu na kuvivuta anaanza kujiamini na kutaka kufanya zaidi ili kuifanyia mazoezi ile nguvu iliyomo ndani yake, na hiyo ndiyo kweli!

“Ni jambo la hekima kutafuta kujua ukweli kuhusu wewe”

Mwanadamu anapotafuta kujua yeye katokea ukoo gani, baba yake na mama yake ni akina nani, mila na desturi zake ni zipi na ana urithi gani kutoka katika familia yake na kutaka kujua wajibu wake ni upi basi huyo anakuwa amefanya jambo la hekima!

Siku utakapogundua kusudi la maisha yako, nani uambatane naye ili ufike wapi, na kwa raslimali zipi na kwa wakati gani hapo ndipo utaanza kuishi maisha yenye tija!

Biblia inasema katika Mithali 23:7a, “Maana aonavyo nafsini mwake , ndivyo alivyo.” Jifunze kujiona vyema na kupenda vilivyomo ndani yako ili kuvipa nguvu.

Jinenee mazuri na kujitabiria siku njema na zenye mafanikio makubwa kuliko jana yako. Usisite kujitabiria mambo mema hata kama uko kwenye kipindi kigumu cha kimaisha na hakika hakuna mwanadamu siyepitia shida hivyo hauko pekeyako wapo watu wengi tu wanapitia uyapitiayo lakini tofauti ni jinsi mtu anavyolichukulia tatizo na jinsi ajionavyo nafsini mwake.

Watu wengi wanapopata changamoto huishia kulaumu ambapo kulumu kunaiua ile nguvu uliyonayo kwani humaanisha ya kwamba umenyoosha mikono na kukubali kuwa hauwezi tena kutafuta jawabu la tatizo husika pia kujionesha kuwa sio kosa lako bali ni kosa la mtu mwingine.

Unapopitia changamoto jiulize "Ni kwa jinsi gani nitavuka?" sio tutavukaje?, usitafute wingi panapopaswa kuwa na umoja. Unapojiuliza swali hilo nguvu iliyoko ndani yako huamka na kufanya kazi kwa namna amabayo hujawashi kuona na hakika haijalishi changamoto ni kubwa kiasi gani lakini utaitatua na kufurahia mafanikio yako.

Unaposema "siwezi" nguvu iliyo ndani yako huenda kulala kwani umeshaipa ruhusa ya kutokufikiria au kutokuhusika tena kwa jinsi gani ikutoe kwenye changamoto uliyo nayo kwa wakati husika.

Mungu aliumba mbingu na nchi kwa neno! Maneno yana nguvu sana hata kwako wewe mwanadamu uliyeumbwa kwa mfano wake yeye aliyekufanya. Unapojitamkia vibaya hakika itakuwa na hakika utakula matunda ya ulimi wako kwa wakati husika! Usikubali kuingia katika mitego ya ujinenea uovu hata mara moja na mitego hiyo hutokea ili uonekane na wewe ni mwanadamu wa kawaida kawaida kama wengine! Kataa hiyo, wewe sio wa kawaida na wala hautakwama kwa uzembe wa maneno yako yasiyo na hekima ndani yake.

Mara kwa mara nikiwa sokoni; nikumuuliza mfanyabiashara kuhusu maendeleo yake, asilimia themanini ya wafanya biashara hujibu kwamba hali ni ngumu sana! Si ajabu ndio maana biashara zao ziko palepale kila mwaka hazina maendeleo yanayoweza kuonekana!

Isiwe hivyo kwako! Kiri mafanikio yaliyoko ndani mwako kabla hayajatokea kwa nje na kuweza kuonekana, kumbuka ujionavyo ndani mwako ndivyo ulivyo!

## Ijenge nafsi yako kwa Uthamani

Kama ni kweli kwamba ajionavyo mtu nafsini mwake ndivyo alivyo, basi yatupasa kuzijenga nafsi zetu vyema ili tujione vyema!

Unapojiangalia kwenye kioo unapaswa kujiona wewe jinsi ulivyo na kioo chako kisikuongezee wala kukupunguzia muonekano wako! Na kama unataka kuonekana au kujiona mrembo ama mtanashati mbele ya kioo kuna mambo mawili ya kufanya. Cha kwanza; yakupasa kukisafisha kioo kwa ustadi na umakini ili kiweze kukupa picha halisi ya muonekano wako pia ukiweke kwenye eneo lenye mwanga mzuri na pia jambo la pili; unapaswa wewe mwenyewe uwe nadhifu. Kwa mambo hayo mawili hakika kioo chako kitakupa muonekano wako mzuri na utakaokufanya ujisikie vyema na mwenye heri!

> Kioo chako ndio nafsi yako; ifanye nafsi yako ikutumikie vyema. Ipe nafsi yako nguvu ya kukuonesha wewe vizuri kila siku unapojiangalia. Maisha yanaweza kuipiga vita sana nafsi yako na ikanyong`onyea na kukosa tena tumaini mpaka ikafikia kufuta picha njema juu ya maisha yako ya baadae na kuishia kuipoza nguvu iliyo ndani

yako! Lakini usiogope na wala usikubali dunia ukupeleke inavyotaka, kataa na jipe nguvu nafsini mwako!

Japokuwa kwa muonekano wa nje unachakaa, amini ya kuwa ndani yako unafanywa upya na bora zaidi. Ukarabati unaofanyika ndani yako hakika matokeo yake yataonekana nje pia wakati utakapowadia.

Nafsi hulishwa; kama unavyoweza kujenga mwili wako kwa kula vyakula bora ndivyo hivyo hata nafsi yako inavyojengwa. Unaweza usijue kwamba ni lini umeijenga kama vile usivyojua ni lini umenenepa baada ya kula vyakula vizuri mpaka pale watu unaoishi nao watakapokuambia au pale utakapokwenda kupima uzito! Utagundua ya kwamba nafsi yako iko imara au ni dhaifu pale utakapopata changamoto ama watu watakapokueleza jinsi wanavyokuona kwa matunda ya kinywa chako maana kimjazacho mtu ndicho kimtokacho. Anayekatisha tamaa wenzie na kuongea maneno yasiyo na hekima hudhihirisha ya kwamba nafsi yake imedhoofika na anapaswa kuiboresha!

Kinachoilisha nafsi yako ni mwenendo wa maisha yako na jinsi ulivyoweka utaratibu wa kufanya mambo yako! Kwa mfano unaposali, unaposoma neno la Mungu na vitabu vingineyo unaijenga nafsi yako kuwa bora zaidi.

Unaposikiliza redio unaifanya nafsi yako kuwa bora ama kuwa dhaifu hapo inategemea unasikiliza kitu chema ama kibaya.

"Yakupasa kuchagua kuipa nafsi yako chakula bora"

Tunazungukwa na taarifa mbaya kila kunapokucha na usipokuwa mtu wa kuchagua utajikuta umeifanya nafsi yako kuwa dhaifu na kuukosa uelekeo unaokupasa! Mimi binafsi nilijiwekea kutokusikiliza mambo yote yanayosikitisha na kukatisha tamaa!

> Nilikuwa na rafiki ambaye nilikuwa nikikutana naye tu anaaanza kuniambia jinsi anayopambana na hali ngumu na matatizo yanavyomuandama. Baada ya muda na mimi pia nikajikuta katika hali kama yake kwa sababu nilikuwa naijenga nafsi yangu nilipokuwa nikimsikiliza. Sikujua kama nilikuwa nikiiua nafsi yangu bila kujua na hakuwa akinijenga bali kuniharibia nafsi yangu!

Wakati mwingine unaweza usijue kama nafsi yako inadhurika mpaka pale utakapogundua ya kuwa hauna tena ubavu wa kuhimili changamoto bali unakubaliana nazo jinsi zinavyokupeleka pia kwa jinsi yako ya kufikiri na kuongea utagundua hauna tena neno la matumaini litokalo kinywani mwako. Ukiona hali hiyo shituka

haraka na uanze kuijenga nafsi yako kwa upya na usiijenge kwa mambo mabaya bali kwa mambo mazuri na yenye thamani!

## Boresha nafsi yako mara kwa mara

Jiwekee malengo  ya kuhakikisha ya kwamba nafsi yako iko salama na inaleta tija mchana na usiku. Kama vile utumiavyo kisu mara kwa mara, kuna muda hua kinapoteza makali yake. Inakupasa ujihakikishie kuwa na ratiba ya kuiboresha nafsi yako kila mara unapopata nafasi hiyo. Wakati mwingine inatuwia ugumu kwa sababu ya mazingira tunayoishi au kufanyia kazi. Kwa mfano inaweza kufika wakati hauna muda wa kujisomea vitabu lakini unaweza kutumia simu yako ya mkononi kusikiliza mafundisho mbalimbali wakati ukiendelea na shughuli zako ndogo ndogo!

Chagua leo kuijenga nafsi yako vyema ili ikusaidie kukupa nguvu ya kuhimili changamoto na pia kukufikisha kwenye ndoto zako za maisha ya sasa na ya baadae.

“Mafanikio ya mwanadamu hayaanzii nje, huanzia ndani yake”

Angalia ni mambo yapi ukiyafanya huwa unaisikia vizuri na yanaamsha morali ya kufanya kazi kwa bidii na ufanisi. Yaandike hayo na kisha uanze kuyafanya mara kwa mara maana hayo ndiyo yanayokufanya uendelee kuwa na nguvu wala sio dhaifu.

Inawezekana ikawa ni kufanya mazoezi ya mwili, kuwasiliana na ndugu na jamaa, kusoma vitabu, kucheza mziki au hata kusafiri. Usikubali nafsi yako ichoke kwa sababu ya magumu unayoyapitia.

Unapoona vita dhidi ya nafsi yako ili kukudhoofisha vimekuwa ni vikali na wewe pia ongeza bidii katika kuiboresha na kutokuacha nafasi kabisa ya mashambulizi kukuathiri wewe! Hiyo itakusaidia na kukupa nguvu ya kuweza kuendelea mbele!

Unapopokea taarifa mbaya chungulia nafsini mwako halafu nenda kapambane mpaka tatizo hilo liishe kwa sababu nguvu unayo na uwezo wa kufanikiwa unao endapo tu utaamua kuutumia na kuhakikisha haurudi nyuma bali unasonga mbele bila kujali ukali wa vita ukoje mbele yako!

Biblia inasema linda sana moyo wako kuliko vyote uvilindavyo maana huko ndiko zitokako chemichemi za uzima wako!

Usipoteze vitu vya msingi rafiki yangu, pambana kupigania utu wako wa ndani kwanza ndipo utaona matokeo bora kwa nje! Wengi wameishia kupigania mambo au vitu vinavyoonekana kwanza ili jamii iwaone kuwa ni bora kumbe wao ni kama maputo tu kwani ndani yao hakuna tumaini wala nguvu tena!

## SURA YA PILI

## SIRI KUU 5 KUHUSU MAJARIBU

Kabla haujayajua hayo mambo matano kuhusu jaribu ni vema ukaweza kujua tofauti kati ya jaribu na tatizo. Fikiria kidogo ni ipi itakuwa tofauti yake! Tatizo ni jambo linalomkumba mwanadamu lakini halimuweki njia panda. Halimfikishi mwanadamu mwisho wa akili zake na humpa njia mbadala na za kutosha ili kulitatua kama akifumbua macho yake vyema.

Jaribu ni jambo ambalo likimfikia mtu huwa anakuwa njia panda hajui kabisa afanye nini na aanzie wapi. Humfanya mtu afikie kufanya maamuzi ya kuacha ama kuendelea. Kufa ama kupona! Yaani kama ni ndoa; kuachana ama kuendelea na mahusiano. Kama ni shule; kuacha elimu ama kuendelea na elimu. Kama ni biashara vivyo hivyo njia mbadala ni mbili pekee aache biashara ama aendelee, hauwezi kwenda mbele wala kurudi nyuma. kama mtu hajafikia hatua hiyo na anaendelea mbele basi huyo ana tatizo tu na wala sio jaribu;

> Wakati mwingine jambo linalofanana linaweza kuwa ni jaribu kwa mwingine na mwingine ikawa ni tatizo tu. Ukiweza kutofautisha hayo mawili

itakupa maarifa bora zaidi wakati unatatua au kufanyia kazi. Sasa ngoja tuzungumze kuhusu jaribu!

Ukweli ni kwamba mwanadamu anapaswa kupitia majaribu na ni muhimu sana kwake. Luka 17:1a inasema "Makwazo hayana budi kuja…..", makwazo maana yake ni yale mambo yote yanayokufanya ujione kama hauendi mbele, uko palepale ama unarudi nyuma ikiwemo matatizo na majaribu. Neno "hayana budi kuja" maana yake ni kwamba majaribu au makwazo ni lazima yaje kwa kiingereza tungesema ni "necessary" yaani ni lazima na ni muhimu.

Kama unajua kwamba kuna mambo ambayo hauwezi kuyabadilisha maishani mwako, hua unachukua hatua gani? Kukubali yaje na uyashinde ama kushindana nayo siku zote za maisha yako ili yasikupate? Biblia inasema katika Yakobo 1:2, "Ndugu zangu, hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali."

Kama wewe ni mwanadamu halisi tambua kwamba majaribu ni kawaida na muhimu sana kwetu pia ni sehemu ya maisha yetu na ukiyakosa maana yeke unadumaa kwani utakuwa umekosa vitamini ya kukufanya ukue! Wakati mwingine tamani vitamini hiyo!

Naamini mpaka sasa tunaweza ingia pamoja kwenye mambo matano ya muhimu kwa mwanadamu kufahamu kuhusu jaribu ili uweze kustahimili na kushinda. Katika 1 Wakorinto 10:13, biblia inasema "Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili." Kupitia mstari huu wa biblia tutatohoa na kuyachambua mambo hayo matano.

## I. Jaribu ni Kawaida ya Wanadamu

Neno linasema "Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu….." Jaribu mpendwa ni kawaida kabisa kwako. Mungu katuwekea mfumo wa kukua kupitia changamoto nasi tukifanikiwa kuzivuka tunakuwa tumekua hakika. Tukizikimbia ndipo tunaanza kudumaa. Sasa jiulize unapokutana na jambo la kawaida maishani mwako huwa unachukua hatua gani? Mimi ninachojua ni kwamba kujiamini kwako huongezeka na wakati mwingine unaweza ukafanyia kazi pasipo hata kuweka akili yako yote hapo. Kwa mfano; unapojisikia njaa maana yake unapaswa kutafuta chakula kwa kupika, kupikiwa ama kununua hotelini. Je, wakati huo huwa unakuwa na hofu?. Hauwezi na wala haupaswi kuwa na

hofu kwani maana unazo mbinu zote za kuweza kutatua na ni mzoefu kwenye jambo lijalo mara kwa mara kwako.

> Kumbuka jaribu huja kukujenga wewe ili uwe bora zaidi hasa utu wako wa ndani na ni utaratibu wa Mungu ili kukufanya ukue vema! Ni sawa na jinsi ambavyo mwanadamu anapaswa kula chakula mara tatu kwa siku. Vivyo hivyo na jaribu lipo ili kukupa vitamini za muhimu ili apate kukua na kuongezeka.

Majaribu huwa na tabia ya kubadilika mara kwa mara kuelekea ngazi kubwa zaidi. Yaani kama leo lilikuwa dogo, kesho litakuja kubwa lakini endapo ukiwa umelishinda la jana. Ni kama mtihani ambapo mwanafunzi asipofaulu leo atarudia tena na tena na tena mpaka pale ambapo atafaulu ndipo mwalimu wake atampa mtihani mwingine wa ngazi ya juu zaidi.

Licha ya hivyo, bado hatuwezi kulifanya jaribu kama kitu kigeni sana kwetu. Kama ulishinda jaribu la jana basi hata la leo utaweza tu kupita ndani yake, kujifunza na kuhakikisha unafanikiwa kuendelea mbele ukiwa bora zaidi. Kumbuka hayakupati pekeyako kila mmoja analo lake kwa wakati wake.

## II. Unaweza Kulimudu

Neno la Mungu linasema, "……ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo…." Maana yake unao uwezo wa kulishinda jaribu unalopitia. Uwezo ulio nao na uwezo wa jaribu linalokusonga ni sawa sawa kilichobaki ni utayari wako tu kupambana na kulishinda. Usipokubali kupambana hakika jaribu litakuelemea. Ukiona jaribu lako ni kama mlima mkubwa basi hata nguvu iliyoko ndani yako ni kubwa vilevile kuweza kuuondoa huo mlima.

> Kubali kuwa mshindi kwani rasilimali zote za kushinda unazo. Na umehakikishiwa ushindi endapo utazifuata kanuni za Mungu wakati unapambana na tatizo ulilo nalo. Kumbuka Efeso 6:12, "Kwa maana kushindana kwetu si juu ya nyama na damu, bali dhidi ya falme, mamlaka, dhidi ya wakuu wa giza na majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho." Hiyo ni moja ya kanuni za kushinda vita vyako ama jaribu lako mpendwa.

Pia katika 2 Wakorintho 10:3, "Ingawa tunaishi duniani lakini hatupigani vita kama ulimwengu ufanyavyo. 4 Silaha za vita vyetu si za mwili, Bali zina uwezo katika

Mungu hata kuangusha ngome. 5 Tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo." Usipoteze muda wako wenye thamani kupambana kwa mwili kama wengine wafanyavyo! Utapoteza vita na utaumia zaidi kuliko unavyoweza kufikiri.

> Kwa kawaida unapoendelea kukiogopa kitu ndipo kitakutesa zaidi. Ila pale tu unapoanza kuja juu na kukiletea upinzani ndipo kitaacha kukusumbua. Nakumbuka nilipokuwa kidato cha pili Pugu sekondari kuna ndugu tuliyekuwa naye darasa moja alipenda sana kuninyanyasa na kuleta usumbufu usiokuwa wa lazima. Nilipokuwa nikimkwepa alifurahi sana na alipokuwa akipata fursa ya kunivuruga anaitumia ipasavyo. Siku moja nikasema moyoni imetosha na mara nyingine alipotaka kuja juu na mimi nikaenda juu zaidi, siku nyingine akaja juu tena na mimi nikapaa juu mara mbili yake nikashangaa kuona yeye ndio kaanza kushuka chini na chini na chini mpaka tukafika mahala tukawa marafiki na hakuna tena aliyekuwa akimsumbua mwenzake.

Maisha unayoyaishi yako mikononi mwako na umepewa nguvu ya kuyamudu huku ukimshirikisha Mungu. Tumia

nguvu iliyo ndani yako vyema nawe utagundua kwamba Mungu hakufanya masihara wakati anamuumba mwanadamu. Siku zote jijengee tabia ya kupambana na woga ulioko ndani mwako ili uwe na uwezo wa kumuendea adui aliye mbele yako pia kumbuka Mungu hakutupa roho ya woga bali roho ya nguvu!

Kuwa mnyonge ni maamuzi yako binafsi!

Wakati unapambana ili uvipige vita vilivyo vema tafuta hekima, ufahamu na maarifa ili uweze kuvuka salama! Unajua wakati unapambana unaweza ukamtingisha mtu aliye pembeni na badala ya kupigana vita moja kwa wakati ukajikuta unapambana vita mbili ama tatu kwa wakati huohuo na sijui kama stamina, kasi na nguvu yako itatosha kukufanya kuwa mshindi.

Kuwa muangalifu ili uwe salama maana adui pia hutafuta ahueni ili apate nguvu za kupambana kwa upya. Jifunze kutoka kwa Bwana maana yeye ni jemedari wa vita! Hakuna vita iliyowahi kumshinda Mungu wetu. Ndio maana anasema katika Mathayo 11:29; "……mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu;……..." kama unataka raha nafsini mwako wakati wa vita na usiokuwa wa vita basi kubali kujifunza kutoka kwa Bwana!

Unaweza ukawa mpiganaji mzuri na bado ukawa na amani, mcheshi, mwenye furaha na unayewasaidia watu. Haimaanishi kwamba ukiwa vitani ili umudu vita vyako basi uonekane na uso uliokunjamana, mkimya na uliyeumizwa. Badili tu fikra zako maana vita vyetu si vya damu na nyama ndugu yangu. Ndio maana biblia katika Mathayo 6:16, "Tena mfungapo, msiwe kama wanafiki wenye uso wa kukunjamana; maana hujiumbua nyuso zao, ili waonekane na watu kuwa wanafunga. Amin, nawaambia, wamekwisha kupata thawabu yao. Bali wewe ufungapo, jipake mafuta kichwani, unawe uso; ili usionekane na watu kuwa unafunga, ila na Baba yako aliye sirini; na Baba yako aonaye sirini atakujazi."

## III. Mungu ni Mwaminifu

Neno la Mungu linasema "……ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo;…….." Mpendwa Mungu ni mwaminifu sana na hapendi hata mmoja wetu apotee yupo karibu sana na wewe wakati unapopitia changamoto. Lakini hujificha ili uweze kufanikiwa kukua. Akiwepo karibu yako muda wote hautajihisi uko peke yako na hautatumia nguvu zote zilizo ndani yako na vita hautavitilia maanani. Lakini katika yote bado yeye ni muaminifu sana!

Mungu ni muaminifu hata wakati ambapo sisi sio waaminifu. Unapokuwa katika vita yako amini kwamba yu karibu na anakuona pia anafurahi kuona jinsi unavyotumia uwezo ulio ndani yako kufanikiwa. Maana yeye ndiye aliyekuumba na anapenda kuona unafanya vyema. Endapo utazidiwa hakika atakuokoa! Mkono wake sio mfupi hata ushindwe kukuokoa! Haijalishi umefika kwenye giza nene kiasi gani yeye Bwana ni muaminifu hataacha ujaribiwe kupita uwezo ulio nao. Na kama vita vyetu ni vya kiroho basi imani ndio silaha yako!

Yeye hutengeneza njia pasipo na njia, hata kama unaona muda umekwisha yeye atawahi tu! Pale unapofikia mwisho yeye ndio anaanza kutenda hakika akili zake hazichunguziki. Muamini yeye maana yeye ni wa kuaminiwa!

Neno la Mungu katika 1 Petro 5:7, linasema "…huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu." Kubali leo kuamini kwamba Bwana ni muaminifu na anaweza kuibeba mizigo yako na anayo shauku leo umtwike mizigo yako maana yeye hujishughulisha sana na mambo yetu.

Hata kama unaona umefika mwisho! Mtwikie Mungu mizigo yako hapohapo mwisho na atakushangaza sana. Utashangaa ukijua ya kwamba Mungu hana mwisho wa kutenda. Mataifa yatetemeka kwa ajabu zake na yeye ni mkuu na ni muumba wa miisho ya dunia. Hata hicho kinachokutesa ni yeye amekifanya! Anao uwezo wa kukifanya butu kisiwe na makali! Na ukavuka salama!

Mungu anao uwezo wa kuwafanya wanaokunyanyasa wakapoteza nguvu za kufanya hivyo pia wale wanaokufanya usilale usiku wakakosa wao usingizi na wewe ukalala salama. Wanaokudai wakatulia mpaka pale utakapokuwa na pesa za kulipa madeni yako yote! Ona hapa Zaburi 76:5-6, “Wametekwa wenye moyo thabiti; Wamelala usingizi; Wala hawakuiona mikono yao watu wote walio hodari. Kwa kukemea kwako, Ee Mungu wa Yakobo, Gari na farasi wameshikwa na usingizi mzito.” Kwa nini una hofu? Pata picha mtu anataka akupige na ngumi halafu ghafla haoni mikono yake! Muamini yeye maana yeye ni wa kuaminiwa ulimwenguni kote.

## IV. Kuna Njia ya Kutokea

Neno la Mungu linasema hivi "………lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili muweze kustahimili." Kumbe njia ya kutokea ipo na iko wazi sana japokuwa haionekani mwanzoni. Ipo njia ya kutokea ili uweze kustahimili, endapo dhoruba ikikuzidi hautafia humo hakika utatoka ukiwa salama salimini. Tumejifunza kuhusu kumuamini Mungu wewe muamini tu na njia atakuonesha nawe utatoka salama.

> Wakati giza nene linapofunika macho yako usihofu wala usilie atafanya njia Yesu wetu. Kumbuka ukuta wa Yeriko ulivyokuwa jaribu kwa wana wa Israeli katika safari yao ya kuelekea kanani, ulibomolewa kwa kwa kelele za shangwe tu. Akili zako zifikapo mwisho na giza kufunika macho yako usihofu wala usilie.

Binafsi nimemshuhudia Mungu akinitoa sehemu ambapo ningeangamia na historia yangu ingepotea na juhudi zangu kuwa ubatili mtupu. Mbele ya nguvu za giza na uchawi bado Mungu alinitetea. Cha muhimu kwako ni kumuweka yeye mbele na hakika atakutengenezea njia pia kukuongoza hata ufike mwisho wa safari yako kwa ushuhuda mkuu. Maumivu unayoyapata leo yatakwisha

na utayasahau lakini usizisahau fadhili zake alizokutendea ukaiona njia ya kutokea. Fadhili za Bwana ni mtaji wakati jaribu jingine litakapokuja kwani litakujengea uthabiti na tumaini lako kwa Bwana halitapotea kamwe.

Mungu anasema katika Isaya 43:2, "Upitapo katika maji mengi nitakuwa pamoja nawe; na katika mito, haitakugharikisha; uendapo katika moto, hutateketea; wala mwali wa moto hautakuunguza." Yaani utakuwa salama na mwenye nguvu. Jiamini wakati unapitia changamoto, jua kwamba yupo yeye aliyeshinda ulimwengu na anakujua vema. Anajua kona zake zote na wapi unapaswa utokee!

> Tabia ya mlango wa kutokea huonekana mwisho wa njia, korido ama chumba. Mlango wa kutokea hauonekani mwanzoni mwa tatizo. Jipe moyo ndugu yangu japokuwa haujauona mlango huo wa kutokea mpaka sasa! Jipe muda zaidi nawe utaziona fadhili kuu za Kristo Yesu. Amini upo mlango, mwambie Mungu akuoneshe mlango na uuone kwa wepesi! Na ukitoka, utatoka kama dhahabu utayasahau yote yaliyokuumiza moyo na kukukatisha tamaa.

Nakumbuka miaka kadhaa iliyopita nilikuwa na uhitaji mkubwa sana wa kifedha. Nilifunga sana kwa maombi na wakati huohuo kodi yangu ya nyumba ya kupanga pia ilikuwa imefika mwisho. Nilipaswa kulipia tena kodi ya pango ama kuhama kabisa. Sikuwa na jinsi nilikuwa katikati sijui nihame ama niendelee kukaa hapo na wakati huo mfuko hauruhusu kuchukua hatua yoyote. Moyoni mwangu nilijisikia kuhama lakini sikujua nitahama vipi!

Nakumbuka nikiwa nimefunga kwa maombi, saa mbili asubuhi ndugu mmoja ambaye nilifahamiana naye ndani ya mwezi mmoja tu alinipigia simu na kuniambia anataka tuonane. Sikujua alikuwa na mpango gani kwa sababu ninapenda kuzungumza na watu nikawa nimekubali wito. Tulipoonana aliniambia ana kiasi fulani cha pesa na hajui akipeleke wapi ili kimletee faida. Hapo ni sawa na kusema "Ng'ombe kafia kwa muuza bucha." Nilimshauri aniazime hiyo pesa kwa riba na akakubali. Ilikuwa ni kiwango kilekile ambacho nilikuwa nakihitaji. Nilimshangaa sana Mungu nakumbuka nilitoka hapo huku nikiwa nanena kwa lugha tu. Kesho yake nikatafuta nyumba nyingine ya kupanga na nikaipata siku hiyo hiyo na baada ya siku moja nikafanikiwa kuihamia.

Mungu hana muda muafaka wa kutenda lakini hakosei wala kukuacha upotee. Mlango wangu wa kutokea

niliuona mwishoni kabisa! Ni neema iliyoje kumjua huyu Yesu! Mimi sina tena mashaka naye, namkabidhi na yeye atatenda kwa wakati wake. Wewe je?!

## V. Lazima Upite Hapo ili Ukue

Neno la Mungu linasema, "Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu….." Kama Mungu anaweza kuruhusu jaribu limfikie mwanadamu basi anamaanisha unapaswa kupita katikati yake. Haupaswi kulikimbia, kupita juu yake, kupita chini yake wala pembeni yake. Ukifanya hivyo maana yake utarudia rudia jaribu hilo hilo mpaka pale utakapoweza kulishinda yaani kuwa jasiri ili kupita katika jaribu hilo. Mungu sio mpoteza muda na wala sio mnyanyasaji mpaka akufanye ufikie hatua uliyonayo sasa bila faida yoyote!

Mwanadamu hujengwa akiwa hapa duniani kwa nyakati tofauti tofauti. Mungu aliyemuumba huratibu hilo ili kwamba mwanadamu aweze kuifikia hatima yake kama vile Mungu alivyoitengeneza. Majaribu hutufanya tukue yaani tutoke katika utoto kuelekea utu uzima kiroho na kimwili.

Kinachomfanya mvulana awe mwanaume ni majaribu! Kinachomfanya msichana awe mwanamke ni majaribu!

> Nchi nyingi zinataabika kwa sababu ya ongezeko la utegemezi hasa baada ya wimbi kubwa la ukosefu wa ajira kwa vijana. Hata wale waliotegemewa kuajiri wenzao na wao wanataka kuajiriwa. Hii ni kwa sababu vijana wengi wanataka njia za mkato na kukimbia changamoto pale ambapo Mungu ameficha hatima zao katikati ya majaribu yanayowapasa wayakabili.

Kijana anaona ni bora akae nyumbani pasipo na ridhiko lakini tu asihangaike kuanzisha ama kufanya chochote kitakachomuingizia kipato! Kukosa ridhiko ndio jaribu lenyewe na Mungu anakutegemea ushinde hali hiyo ili ukafanikiwe uendako lakini bado kijana anakuwa mgumu kupitia chanagamoto hiyo na ndio maana tuna wanaume wengi wenye miaka arobaini na bado hawajakua kiakili kwani wamekataa kuishinda mitihani hiyo.

Nakusihi kijana mwenzangu upitiapo changamoto amini huko ndiko kukua kwako na ndiko kuinuliwa kwako. Utakapokimbia changamoto ni wewe mwenyewe ndio unajichelewesha! Fika mahala anza kukabili mambo unayoyaogopa nawe utakuwa huru daima! Kujaribiwa kwako kunakujengea ustahimilivu kama vile Yakobo 1:3, inavyosema "Kwa maana mnafahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu hujenga ustahimilivu." Kama

unataka kuwa mstahimilivu basi kubali kujaribiwa mpendwa, nje ya hapo ni kwa neema tu.

Mstari wa nne unasema "Na ustahimilivu ukimaliza kazi yake mtakuwa wakamilifu pasipo kupungukiwa na chochote." Sasa umejua ili uwe mkamilifu na usipongukiwe na chochote basi tii maagizo mpendwa! Amini sasa, anza kutendea kazi sasa.

Nakumbuka nilikuwa kwenye uhitaji wa fedha ya haraka ili niweze kutimiza jambo fulani! Nakumbuka usiku ule tulimuomba Mungu nikiwa na mke wangu tukasema "Mungu wa madhababu tunayoabudia tunaomba utujibu na ujidhihirishe." Kesho yake asubuhi sana nikapigiwa simu na shirika moja la kimataifa lililokuwa na uhitaji wa baadhi ya mambo ili kukamilisha shughuli zao. Nilipokwenda kutoa huduma yangu ghafla wakagundua kuwa nina uwezo wa kuzungumza na wananchi kuhusu jambo fulani na nikaweza kuzungumza kuuza vitabu vyangu kwa wingi pia. Hivyo nililipwa maradufu!! Nikapata pesa yote niliyokuwa nahitaji pamoja na ya ziada.

Mungu hakuishia kunipa pesa tu bali alitaka nifahamike kimataifa. Changamoto ile ilinikuza na kunifanya jina langu lisikike ulimwenguni na pia ikafungulia na baraka zingine tele.

# SURA YA TATU

# MAMBO YA KUFANYA UNAPOPITIA KWENYE JARIBU

Jaribu humfanya mwanadamu ukosa uelekeo na hatimaye kukaa chini na kuchutama akiwaza aende wapi na afanye nini pasipo na faraja yoyote wala matumaini yoyote. Mungu hujificha na kuonekana yuko mbali kuliko nyakati zote lakini ukweli ni kwamba wakati wa jaribu Mungu huwa karibu zaidi na mwanadamu.

Pale unapojikuta umekata tamaa na haujui ufanye nini na pengine kujiua ndio jawabu ulilobakiza haya mambo matano yatakusaidia wakati wa jaribu lako. Utavuka salama na utakuwa bora zaidi kuliko awali kwani jaribu ni sehemu ya maisha ya mwanadamu ili apate kukua na kuongezeka;

## Endelea Kuwa na Fikra Njema

Akili yako imepewa nguvu ya kuamua matokeo ya chochote unachopitia na pia kuijenga hatima yako! Maana neno la Mungu linasema  katika Mithali 23:7 “Maana aonavyo nafsini mwake, ndivyo alivyo.” Hauwezi kuwa bora zaidi ya ujionavyo nafsini mwako.

Na jinsi ujionavyo nafsini mwako ni vile ambavyo unavyoyafikiria maisha yako, changamoto yako, na hata hatima yako.

Unapokuwa na fikra njema utaweza kuwa na amani wakati wa jaribu lako. Mtumishi wa Mungu Yohana alipokuwa katika kisiwa cha mateso kisiwa cha Patmo aliona mbingu mpya na nchi mpya vikishuka; katika Ufunuo 21:1 "Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya;…….” Wewe unaona nini wakati unapopitia kwenye changamoto? Je, ndio wakati unapowawaza sana maadui na watesi wako ama ndio wakati unaouona ukuu wa Mungu juu yako na kuthibitisha ya kuwa una nguvu juu ya yote yanayokukabili?

Usipokuwa makini utafananishwa na tembo aliyefungwa
kamba mguuni halafu ikaunganishwa na kidumu kidogo
cha lita tano za maji na tembo huyo akaamini kuwa
hawezi kabisa kutoka kwenye kifungo hicho.

Ni kweli kabisa kwamba jaribu huwa halina sura nzuri, wala halioneshi kwamba unaliweza na wakati mwingine hujitambulisha kwako kwa shuhuda ya kuwamaliza wengine wengi kabla yako. Siri moja kuu ni kwamba “yategemea wewe utaamua nini, hata kama jaribu lije kwa fujo na makelele kiasi gani.” Tena kwa mtu mwenye

hekima utagundua kwamba pale ambapo kelele ni nyingi zaidi ndipo pana debe tupu.

Usikiri chochote kiovu juu yako! Unapokubali kitu kiovu na kukikiri kwa kinywa chako biblia inasema hivi katika Mithali 6:2, “Basi umetegwa kwa maneno ya kinywa chako, Umekamatwa kwa maneno ya kinywa chako.” Mungu anaweza kuwa na mpango mwema juu yako tena wa kukuokoa na kukuweka huru kutoka kwenye jaribu lako lakini endapo wewe mwenyewe usipokiri kufanikiwa ama kushinda kwako hakika utabaki palepale.

Sio lazima wakati wote uwaeleze watu unachokipitia. Hapo ndipo shetani humtega mwanadamu kwani utakayemueleza tatizo lako kama sio jasiri ama mkomavu atakukatisha tamaa na wewe utajikuta unakiri kukata tamaa. Silaha yako iko katika Mithali 10:19 “Katika wingi wa maneno hapakosi kuwa na kosa, lakini anayezuia midomo yake anatenda kwa busara.” Jitahidi kuzuia midomo yako wakati ambapo hauna uhakika kama utanena kitu ambacho ni sahihi kwa ajili yako na hata kwa yule unayemuambia. Mara nyingine unaweza kujikuta unamueleza mambo makubwa mtu ambaye bado imani yake ni changa na hajafikia hatua hiyo ya kukua.

Umepitia hali hiyo kwa sababu ndio wakati wako kupitia hapo, unayemueleza sasa yawezekana

atafikia hatua hiyo baada ya miaka mitano ijayo, huyo atakudidimiza zaidi. Enenda kwa hekima na ukiwiwa kueleza tatizo lako basi mueleze mtu ambaye tayari amepitia hapo ili akushike mkono na kukuvuta nje ya shimo hilo.

Hakikisha unajijenga kwa mambo ambayo ni mema, yanayokupeleka hatua nyingine mbele na wala sio kukurudisha nyuma kifikra! Ukiwa karibu na watu wenye mawazo hasi ni hasara kubwa kwako. Jitenge nao!

Kumbuka Mungu aliumba mbingu na nchi kwa neno, nasi tu mfano wa Mungu hivyo tutamkapo; nchi na mbingu zinasikia na kutekeleza yote tutamkayo. Uamkapo asubuhi kiri na tamka ya kuwa "Hakika wema na fadhili za Bwana zitakufuata wewe siku zote za maisha yako, nawe utakaa nyumbani mwa Bwana milele na milele. Amina!"

## Omba kwa Bidii

Unapopitia jaribu mpendwa silaha yako ni maombi na tena maombi yana nguvu za kumshinda mtesi wako ibilisi. Yakobo 4:7b inasema "……Mpingeni shetani, naye atawakimbia." Utakapochukua hatua ya kumpinga shetani katika maombi hakika atakimbia na kukuacha salama. Unapopitia changamoto ni Mungu pekee ajuaye

unapaswa kufanya nini ili utoke hapo. Ni wakati bora zaidi kumkaribia Mungu ili akupe maelekezo yake na uyafuate.

Omba kwa bidii sana maana neno linasema maombi ya mwenye haki yanafaa sana kama akiomba kwa bidii. Maombi kwa mKristo hayapaswi kuwa wakati wa majaribu pekee bali yapaswa kuwa ni sehemu ya maisha yake mchana na usiku, tena kwa bidii ndio maana Yesu aliwaambia wanafunzi wake "kesheni mkiomba msije mkaingia majaribuni."  Chagua kumuomba Mungu ili uwe salama. Jiachilie kwake na umuamini. Hakika atafanya!

Usisite kumuomba hata kama unaona kilichokupata sio haki yako, umeonewa na wala haukustahili kabisa. Neno la Mungu linasema katika Yakobo 5:13a, "Je, kuna mtu ye yote miongoni mwenu aliye na shida? Basi na aombe…." Usisite kuomba hata kama hauoni mlango wa kutokea. Hauwezi kuuona mlango wa kutokea kabla haujafika mwisho mpendwa! Vumilia kidogo tu nawe utauona mkono wa Bwana kukuokoa na kukupongeza kwa ushindi mkuu na ustahimilivu uliouonesha. Kumbuka mkono wa Bwana sio mfupi kukugusa na wala sikio lake sio zito hata asiweze kusikia maombi yako.

Wakati wa jaribu lako unapaswa kumtumaini Mungu pekee kama neno lake lisemavyo katika Mithali 3:5-6 “Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, Wala usizitegemee akili zako mwenyewe; Katika njia zako zote mkiri yeye, Naye atayanyosha mapito yako.” Chagua kumtumainia Bwana nawe utakuwa kama mlima Sayuni na hautatikiswa na jaribu lako, litakuja na litakuacha salama na ukiwa mwenye nguvu zaidi.

Lakini yakupasa kujua ya kwamba kinachopasa kukupeleka kuomba isiwe ni changamoto uliyonayo bali iwe ni neno lake. Unapopata shida usikimbilie kuomba bila kusoma na kutafakari neno lake. Chunguza Mungu amesema nini kuhusu unalopitia ndipo uende ukamuombe yeye ukiwa na ufahamu na maarifa! Neno la Mungu linasema katika Yeremia 1:12b, “…..kwa maana niko macho kuhusu neno langu ili kulitimiza.” Mungu yuko makini sana kwenye kutimiza neno lake. Na hulituma neno lake ili kutuponya katika masumbufu yetu yote.

> Unapopata tatizo tafuta mahala ambapo neno linaelezea tatizo kama lako halafu amini kuwa Mungu anaweza kukusaidia na kukutoa katika tatizo kama hilo halafu ingia kwenye maombi ukiwa umelishika neno la Mungu.

Muombe Roho Mtakatifu akuwezeshe kunena kwa lugha maana yeye Roho wa Mungu hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa. Unapoomba kwa akili zako hauwezi kuwa mtimilifu katika maombi yako maana Roho wa Mungu atujua vema sana na anajua matatizo tuliyonayo. Katika 1 Wakorinto 14:15, biblia inasema "Nifanyeje basi? Nitaomba kwa roho na nitaomba kwa akili yangu pia. Nitaimba kwa roho na nitaimba kwa akili yangu pia." Usikubali kuitegemea akili yako pekee katika maombi. Mshirikishe Roho Mtakatifu maana neno linasema kwamba wanaaongozwa na Roho ndio wana wa Mungu. Roho Mtakatifu akikuongoza katika maombi yako hakika utakuwa na amani na furaha tele. Kuishi katika mwili ni mauti bali kuishi katika Roho ni uzima na amani.

Kama unapenda uzima na amani katika maisha yako yote basi jifunze kuongozwa na Roho wa Mungu! Ni amani na furaha tele maana maongozi yake ni ya upendo na neema tele! Utajikuta umepata vitu ambavyo haukuvitarajia kuvipata maishani mwako na wala hata ndugu zako hawakuweza kuvipata! Tena utavipata kwa wepesi!

## Amini Kwamba Utashinda

Imani ni silaha kubwa ya mKristo anayeishi katika ulimwengu huu wa sasa! Neno la Mungu linasema katika Waebrania 11:1, “Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.”  Kama mKristo unapaswa kuwa na hakika na Mungu wako. Usimchukulie kwa kawaida kawaida kwani yeye si wa kawaida. Muamini kwa kiwango cha juu sana mpaka wewe mwenyewe ushangae.

> Muamini Mungu katika mambo yote unayoyatarajia kana kwamba tayari yamekwisha kuwepo ama kufanyika. Amini Mungu amekuponya tayari huo ugonjwa ulio nao hata kama bado unasikia maumivu. Amini biashara yako inakua hata kama unaona imekwama. Mungu hufarahishwa na imani uliyonayo! Amini Mungu anapambana sana na adui zako hata kama unawaona wana furaha kubwa kuliko uliyonayo na hata kama bado wanakuundia njama amini tu kwamba tayari wameshindwa kabisa! Mungu huiangalia imani yako juu na yake ndipo hutenda makuu.

Ni dhambi kubwa kwa mKristo kuishi pasipo imani. Jaribu kujiuliza, wewe ulishawahi kumuona Yesu kwa macho? Mungu je? Ibrahimu je? La hasha! Wote hao haukuwaona lakini kwa nini bado unaamini kuwa wapo ama walikuwepo? Ni imani! Sasa kwa imani hiyohiyo unapaswa kuliamini na neno lake. Ukiweza kuwa na imani ndogo tu unaweza kuhamisha milima rafiki yangu. Unaweza kufanya makuu kupita ufahamu wako ukiwa na imani.

Neno la Mungu linasema katika Waebrania 1:6 “Basi, pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu.” Hii ni sahihi na ni hakika. Uchaguzi ni wako mpendwa uishi kwa imani ama uishi kwa kutegemea akili zako mwenyewe. Hautaweza kuendana na mipango ya Mungu kama hauna imani. Hautaweza kumtii Mungu kama haumuamini. Fungua macho yako leo na gundua kwamba msongo wa mawazo ulio nao unasababishwa tu na kukosa imani kwako. Mungu amesema katika neno lake ya kwamba umtumaini Bwana kwa moyo wako wote na wala usizitegemee akili zako mwenyewe. Ukitegemea akili zako mwenyewe unajitafutia kifo mpendwa, msongo wa mawazo sio sehemu yako. Jifunze kumkabidhi mambo yako, umuamini na hakika atafanya!

Ili uweze kuishi kwa amani kama mKristo ni lazima ujifunze kumtegemea Mungu kwa asilimia mia moja. Usidanganyike na maneno ya watu kwamba Mungu amekwisha kukupa kila kitu hivyo yakupasa kujitegemea mwenyewe. Huo ni uongo mkubwa na wote wafuatao njia hiyo wameangamia na wataendelea kuangamia. Maisha yao yamekosa amani na utulivu.

Neno la Mungu katika kitabu cha Waebrania 10:38 linasema “Lakini mwenye haki wangu ataishi kwa imani; Naye akisita-sita, roho yangu haina furaha naye.” Je, unasitasita? Ukifanya hivyo Bwana hana furaha na wewe kabisa! Hakufurahii tena kwa sababu haumuamini!

> Unajisikiaje wewe kama mwanadamu usipoaminika wakati ambapo ndani yako unajiona kuwa mwaminifu? Naamini unajisikia vibaya sana. Je, si zaidi sana kwa Mungu wetu? Mtu wa Mungu ni lazima aishi kwa imani na nje ya hapo yeye sio mwana wa Mungu na amejitoa mwenyewe!

Umuombapo Mungu ndugu usiwe na shaka kabisa uwe na amani na hakika atakufurahisha. Usikubali kuyumbishwa na chochote hata kama ukimuona adui ameinua silaha zake tayari, amini kwamba Mungu anaweza kuzifanya silaha zake kumpiga yeye

mwenyewe! Neno lake Mungu katika Yakobo 1:6-7 linasema “Lakini aombe kwa imani pasipo shaka yoyote; maana mwenye mashaka ni kama wimbi la bahari ambalo husu kumwa na upepo, likitupwa huku na huku. Mtu kama huyo asidhani atapata kitu cho chote kutoka kwa Bwana;” Ni sikitiko kubwa sana pale ambapo mwanadumu anapoyumba huku na kule kwa maana hata waswahili walisema “Mtaka yote, hukosa yote.” Hauwezi kuitumikia akili yako na Roho wa Mungu kwa wakati mmoja. Mkabidhi Mungu yote na yeye atakuthibitishia kwamba ni wa kuaminiwa. Nje ya hapo usitegemee chochote kutoka kwa Bwana!

## Kaa Karibu na Watu Wanaokutia Moyo

Dunia imejaa watu aina mbalimbali na kila mmoja ana uwezo wa kukuinua ama kukushusha chini. Wewe ni kiumbe ambacho kinapaswa kulelewa ili kikue. Anayekulea akiwa ni bora basi utakuwa bora na endapo anayekulea atakuwa wa hovyo basi hakika na wewe utakuwa wa hovyo. Neno la Mungu linasema mazungumzo wabaya huharibu tabia njema. Hata kama unauwezo mkubwa kiasi gani kutokubaliana na mazungumzo ya wanaokuzunguka; nakuhakikishia ipo siku pasipo wewe kujua utakuwa na mawazo au mazungumzo sawa na wao.

Dawa ya kukuweka salama ni kujiepusha nao kabisa! Simaanishi uwafuate na kuwaambia kwamba sasa unajitenga nao, la hasha! Cha kufanya usiwape muda wako. Baada ya muda na wao watakuacha. Itakufaa nini uwe na marafiki wengi na mwisho wa siku usifikie malengo ama kusudi ambalo Mungu wa mbinguni amekuumbia? Kosa sio lao bali ni lako wewe kwa kushindwa kufanya maamuzi sahihi.

Unapokuwa unapitia changamoto ni wakati mzuri pia wa kujua nani ni halisi kwako na nani ni mnafiki! Tumia wakati huo kuwagundua na kujitenga kabisa na marafiki wanaokuwa na wewe wakati wa raha tu baki na wale watakaojitoa kwa ajili yako. Watakaoamua kufunga na kuomba kwa ajili yako, kukufariji na kuhakikisha hauangamii katika unalopitia ili mfikie malengo kwa pamoja.

> Kuna baadhi ya marafiki watakuja juu yako na kutumia udhaifu wako ili wao wapate nafasi ama umaarufu. Usipange kupambana nao, wasamehe na umuamini Mungu kwamba hapo utavuka tena utakuwa mkuu zaidi yao kwa mara nyingi zaidi ya mwanzo. Unapokuwa kwenye changamoto unapata nafasi ya kukua! Hivyo ukitoka hapo hakika utakuwa mkuu kupita hapo mwanzo.

Tafuta watu ambao wamekwisha kupita na kufanikiwa kuishinda hali hiyo uliyonayo ili wakushike mkono na wakuelekeze njia ikupasayo kuiendea. Usitafute ushauri kwa watu wasiokuwa na maarifa kuhusu kile ukipitiacho. Usijaribu kutafuta maarifa kwa watu ambao uko nao kwenye ligi moja, wengi wao waakukatisha tamaa na kukukosesha amani ili wao waendelee mbele wakati wewe umekwama. Badala ya kukupa mkono watakudidimiza kwenye matope ili upotee kabisa! Hauwezi ukamjua adui yako kwa wepesi, hivyo ni vema kama ukiamua kukaa kimya na kumtegemea Mungu.

## Nani Anafaa Kukushauri?

Kuna maeneo makuu matatu ya kuaminika ili uweze kupata ushauri mzuri wa kukutia moyo na kukuvusha katika changamoto yako ni;

**Kwanza;** Kiongozi wako wa kiroho! Nenda kamueleze shida yako kwa kuwa ana hekima ya Mungu itokayo juu na ana uzoefu wa kutatua changamoto za watu mbalimbali anaowaongoza. Muamini na atakupa ushauri uliobora kwani ana kuombea na uko chini yake kama kondoo ili akuchunge.

Ni wajibu wake kuhakikisha kwamba wote walio chini yake wapo salama na wanaendelea vizuri kiroho na

kimwili hivyo atajidhatiti kuhakikisha umefanikiwa kuivuka changamoto yako. Ni sawa na mchungaji wa kondoo, hupenda kondoo wake wote wawe na afya njema na atahakikisha wamekula na kunywa vizuri.

**Pili;** Mzazi au mlezi wako, watu hawa Mungu husema nao kuhusu maisha yako tangu ulipokuwa mdogo. Wanakujua udhaifu wako na uwezo wako wa kuhimili changamoto zinazokusonga. Unachokosea ni kuwaficha unachokipitia! Pengine jambo unalopitia walijua ama wanajua kwamba utalipitia ukifikia umri fulani na wakawa hawajakueleza kwa sababu ulikuwa bado mdogo.

Wakati mwingine unalopitia ni kawaida kwenye familia yenu na wanajua nini cha kufanya ili upone. Mungu ameumba viumbe vyote na akavipa nguvu ya kufundishana namna ya kuishi. Pale ambapo unafundishwa na mzazi wako ama mlezi wako na ukapuuza ndipo unapojitakia maangamizo yako mwenyewe! Kubali kutii ili siku zako za kuishi ziongezeke kwani wao wanajua. Kwa mfano; familia yako ina gonjwa la Pumu ambalo ni la kurithi na wazazi wako wamekusihi usipende kukaa maeneo yenye baridi ama upepo mwingi kwa muda mrefu na wewe

ukaendelea kufanya uonavyo kuwa ni vyema hakika siku zako za kuishi zitapungua.

**Tatu;** Roho Mtakatifu, huyu ni msaidizi ambaye Bwana Yesu alituachia. Roho mtakatifu ni Mungu, sehemu ya tatu ya utatu wa Mungu. Kama Mungu, Roho mtakatifu anaweza kufanya kazi ya msaidizi na mshauri kama vile Yesu Kristo alivyoahidi kuwa atakuja kufanya. Kama vile kitabu cha Yohana 14:16 kisemavyo "Nami nitamwomba Baba, naye atawapeni Msaidizi mwingine akae nanyi siku zote. Huyo ndiye Roho wa Kweli ambaye watu wasioamini hawawezi kumpokea." Roho mtakatifu atakujilia endapo utachagua kumuamini. Hapendi kukaa mahali ambapo haaminiki.

Ukimuamini atakushauri vema tena atakupa maelekezo ambayo sio ya kubahatisha! Atakupa ufahamu ambao utakutoa kwenye shida yako kwa namna isiyokuwa ya kawaida nawe utashangaa. Neno la Mungu linasema katika Warumi 8:5 kwamba "Kuishi kwa mwili ni kifo bali kuishi kwa Roho ni uzima na amani." Tuchague kuishi kwa Roho ili tuwe na uzima na amani. Ushauri wa akili yako au mwili wako hautendi haki ya Mungu! Mungu anakusihi uenende kwa Roho ili usitimize tamaa za mwili kwa sababu mwili hutamani ukishindana na Roho. Lakini Roho akiongoza hauko chini ya sheria.

## Usiogope

Woga ni adui mkubwa sana kwa wanadamu. Woga humfanya mwanadamu kukosa amani, furaha na hata kukosa uzima. Aushindaye woga hakika ameshinda vita kubwa sana! Atakuwa ameshinda vita kubwa kwa sababu nafsi ya mwanadamu inapaswa kuwa na chaguo moja kati ya woga na imani. Kama ukiwa hauna woga maana yake imani yako ni kubwa juu ya Mungu wako. Kama hofu kwako ni kubwa basi imani yako kwa Mungu ni ndogo. Hauwezi ukawa na imani kubwa na hofu kubwa wakati huohuo; wala hauwezi kuwa na imani ndogo na hofu ndogo wakati huohuo bali kama imani ni kubwa hofu itakuwa ndogo na kama hofu ni kubwa basi imani yako itakuwa ndogo. Chagua imani kubwa!

Kama mkristo ni vema ukatambua a kwamba Mungu hapendezwi na uoga wako. Katika kitabu cha Ufunuo 21:8, biblia inasema “Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti.” Wewe kuwa muoga sio kwamba umejiepusha na ziwa la moto bali umejipeleka ili ukaangamie. Halafu unaweza kujiuliza, ni nani aliyekufundisha kuwa muoga? Mbona Mungu anakufundisha kuwa jasiri? Na neno lake linasema

hakutupa roho za woga bali za nguvu. Nani ni mwalimu wako?.

Kataa uoga ndani yako na ujenge imani kuu ndani yako juu ya Mungu aliyekuumba. Unapoliogopa jaribu lako unamchukiza Mungu na hakika hautaingia mbinguni kama wewe ni mtu wa hofu nyingi. Hata kama jaribu linakutesa kiasi gani usikubali hofu ikuingie. Utaishia kushindwa na kumlaumu Mungu pasipo na sababu ya msingi wakati wewe ndio chanzo cha kushindwa kwako. Neno linasema katika Yakobo 1:5-8, “Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.” Unapoenda mbele za Mungu amini kwamba yupo na uwe na imani juu yake. Neno la Mungu linasema “Angalieni vizazi vya kale mkaone: nani aliyemtumaini Bwana akaaibika Nani aliyekaa hali ya kumcha akaachwa? Nani aliyemwita akadharauliwa?.” Hakika ukiwa na imani, ukamuita Mungu utakuwa salama!

> Ijenge imani yako katika neno la Mungu maana ndio msingi wa uKristo. Neno lake ni hakika na kweli. Imani huja kwa kusikia neno la Mungu. Ukiamua kumsikiliza Mungu katika neno lake hakika utakuwa na imani kuu.

Mungu anasema katika Isaya 43:2, “Upitapo katika maji mengi nitakuwa pamoja nawe; na katika mito, haitakugharikisha; uendapo katika moto, hutateketea; wala mwali wa moto hautakuunguza.” Yaani utakuwa salama na mwenye nguvu. Wana amani tele walio ndani ya Kristo Yesu. Jiamini wakati unapitia changamoto, jua kwamba yupo yeye aliyeshinda ulimwengu na anaujua vema. Anajua kona zake zote na wapi unapaswa utokee!

# SURA YA NNE

## USIPOTEZE MUDA

Jaribu limjiapo mwanadamu humpunguzia ufanisi katika kutimiza majukumu yake ya kila siku kifamilia, kijamii na hata katika mambo yanayomuhusu yeye mwenyewe. Shetani hutumia hicho kumfanya mwanadamu kuwa mzembe na kupoteza muda mwingi kwa kukaa nyumbani akiwa anaugulia tatizo lake. Lakini neno la Bwana linatusihi tuenende huku tukiukomboa wakati. Hata kama ni kipindi kigumu bado yakupasa tu kuukomboa wakati. Unahitaji kuukaza mwendo wakati huohuo ukipambana na magumu unayoyapitia.

> Maisha yanafananishwa na uendeshaji wa baisikeli. Ili pawe na uwiano na usianguke yakupasa uendeshe; yaani uwe kwenye mwendo na mwendo wenyewe ni kwenda mbele. Endapo utasimama basi uwe na uhakika utaanguka chini.

Wakati wa tatizo lako sio wakati wa kusimama, ni wakati mzuri wa kuendelea kusonga mbele! Sio wakati wa kujifungia ndani! Sio wakati wa kugombana na majirani zako! Sio wakati wa kupoteza muelekeo! Usidanganyike kwamba maisha yanaweza kusimama mahala pamoja

ama kutia nanga, la hasha! Kama vile muda usivyosimama na wewe pia hauwezi kubaki mahala pamoja; Kuna mawili tu; unaenda mbele ama unarudi nyuma! Kujifungia ndani hakukufanyi uwe mahala pamoja bali hukufanya kurudi nyuma kimaisha hata kama haujigundui kama unarudi nyuma. Ni vema ukatambaa kama hauwezi kutembea, ni vema ukatembea kama hauwezi kukimbia lakini usibaki hapohapo ukiwa unaugulia maumivu yako, kataa!!

## Usijiulize Itakuwaje

Usipoteze muda wako kujiuliza itakuwaje, swali hili huwapotezea watu wengi nguvu ya kupiga hatua! Kama akili yako imejaa imani angalau unaweza kupata majibu mazuri kuhusu matokeo ya unalolipitia; lakini kama wewe ni mtu wa hofu basi swali hilo litakukosesha amani na utajawa na hofu na mwisho wa siku utajifungia ndani.

Jifunze kujiachilia kwa Bwana na kuamini kwamba yeye anafanya mambo makuu kuliko yale ya mwanadamu na akili zake hazichunguziki pia ahadi zake ni za kweli daima.

Swali la muhimu kujiuliza wakati wa changamoto yako ni "Nifanye nini wakati huu?" swali hili lina thamani na msaada zaidi kuliko kujiuliza "itakuwaje?"

Unapojiuliza nifanye nini hapo akili yako itaanza kukupa mawazo tofauti tofauti huku ukimshirikisha na Roho Mtakatifu ili kuhakikisha haukosei tena katika maamuzi yako. Utapata mawazo chanya yatakayokufanya upate tena amani ya kuendelea mbele pasipo kukata tamaa!

Kumbuka kuwa akili yako inaweza kukupa majibu mazuri sana kama ukiitengenezea tabia ya kufikiri kuliko bora! Jinsi akili yako inavyochakata mambo mbalimbali ndivyo wewe unavyojengeka. Kwa mfano; ukijijengea kutokukurupuka katika maamuzi ndivyo utakavyoishi na maamuzi yako yatakuwa bora na yenye tija. Kama utajijengea kufikiria chanya kwa kila jambo basi itakuwa ni ngumu sana kwako kuwa na maisha yenye matokeo hasi.

Unapojiuliza itakuwaje unaruhusu wimbi kubwa la mawazo yanayoleta hofu moyoni mwako! Kwa mfano; unapokuwa unaumwa halafu ukajiuliza itakuwaje. Moja kwa moja utapata mawazo umezidiwa na utakufa. Halafu itakuwaje inachukua hatua ya pili; umeacha watoto wanateseka na hawana msaada! Ona sasa jinsi ambavyo swali itakuwaje linavyoweza kukuletea hali ngumu na kutengeneza picha mbaya akilini mwako na zenye kukatisha tamaa.

Muamini Mungu kwamba anafanya jambo jema kimya kimya, anakutengeneza upya ili uwe kifaa bora zaidi kwa ajili ya utukufu wake. Kazi yako ni kumuuliza kwamba "nichukue hatua gani wakati huu?" Mfalme Daudi na jeshi lake walirudi kutoka vitani akakuta makazi yao yameharibiwa, mali na wake zao wametekwa nyara.

Daudi akaamua kumuuliza Mungu swali "Nifanye nini wakati huu?" yaani "Nikiwafuatilia adui zangu nitawapata?" na Bwana akamjibu na kumruhusu aende na hakika atawapata ndipo katika Zaburi 18:37-38, Daudi alisema "Nitawafuatilia adui zangu na kuwapata, wala sitarudi nyuma hata wakomeshwe, nitawapiga-piga wasiweze kusimama, wataanguka chini ya miguu yangu."

Ingekuwaje kama mfalme Daudi angeanza kujiuliza "itakuwaje?" Nadhani angepoteza muda kwa kukaa chini na kulia kwa uchungu sana kwani wake zao na mali zao zilikuwa zimechukuliwa na wavamizi! Daudi akajipa moyo katika Bwana na akamuuliza kama ataweza kuwapata adui zake na hakika akawapata na kumtukuza Mungu.

## Fanya Jambo Mbadala

Mungu hawezi kukunyima yote wakati wa changamoto yako mpendwa! Utajaribiwa eneo moja na eneo jingine litakuwa wazi kwa ajili yako ili kuweza kukupa ahueni. Wakati wa jaribu lako silaha kubwa ni imani. Ukiwa na imani hakika utapita kwenye magumu, utashindalakini amani ya Kristo haitapungua kwako!

Endapo utaamua kutokuyajali maumivu unayoyapitia na kufurahia upande mwingine wa maisha yako; hapo utaipa nafsi yako nguvu ya kukupeleka katika hatua nyingine ya kuishi vema bila kupoteza muda! Uchungu huzuia maendeleo ya mwanadamu. Maumivu makali ya nafsi na kilio cha mara kwa mara hudhoofisha akili yako na nguvu iliyo ndani yako pia hupooza!

Wakati wa changamoto yako; jaribu kuangalia uwezekano wa wewe kuwa katika mwendo bila kuupoteza muda kwa kukaa ndani na kulia. Mwili wa mwanadamu hupata nguvu zaidi kwa kadri anavyojishughulisha sio kwa kukaa ndani na kujifungia.

“Unapokuwa umelegea eneo moja tafuta eneo jingine ambalo una nguvu”

Usikubali kupigwa kote kote!

Endapo jaribu lako ni kufukuzwa ama kusimamishwa kazi; umekaa nyumbani unalia, unahangaika huku na kule na mwisho wa siku unaona kama umeachwa na dunia imekukataa unaamua kujifungia ndani na kuangalia televisheni mchana kutwa, si vema! Nadhani huo ni wakati bora sana kwako kufanya yale mambo ambayo ulikuwa hauwezi kuyafanya wakati ulipokuwa na shughuli nyingi kazini. Unaweza kutumia muda huo wa jaribu lako kutengeneza bustani hapo nyumbani pakapendeza zaidi. Unaweza kutumia wakati huo kuboresha mahusiano na mwenzi wako wa kimaisha!

> Usikubali kupigwa na adui kila mahala! Unaweza kuamua kusaidia kazi za nyumbani kwa weledi zaidi. Unaweza pia kuhakikisha unatumia muda huo kufuatilia maendeleo ya kimasomo ya watoto wako na kuwafundisha watoto wako neno la Mungu! Chukua jembe palilia majani yanayozunguka nyumba yako! Tengeneza mitaro iliyoziba! Nenda kafagie na kudeki kanisa! Ondoa buibui ndani ya nyumba!

Unaweza kutumia muda huo kwenda kuwatembelea ndugu jamaa na marafiki ambao umepotezana nao kwa muda mrefu na kudumisha urafiki ama undugu wako

kwao. Hakika utajisikia haujapoteza, bado uko kwenye mwendo!

Jaribu lako laweza kuwa ni ugonjwa unakusumbua; muda huo usikubali kulala kitandani tu bali angalia jambo lolote ambalo unaweza kulifanya ili kukuweka katika mwendo bila kupoteza muda wako wa muhimu hata hapo hapo kitandani. Kwa mfano; unaweza kuutumia muda wa ugonjwa wako kusogea karibu zaidi na Mungu kwa kusoma neno lake katika hali ya utulivu zaidi na kumuomba yeye! Unaweza kutumia muda huo kuandika kitabu fulani ambacho kitawasaidia watu wengi kwenye jambo lolote ambalo una ujuzi nalo ikiwemo mapishi, ndoa na hata ujasiliamali.

Kuna kazi ndogo ndogo kama vile kufuma kitambaa, kazi hizi zitakusahaulisha kama unapita kwenye magumu, utakuwa huru kama wengine na utajikuta tu tayari umefika mwisho wa jaribu lako. Wakati huo wote jiachilie kwa Bwana na umwamini kwamba anatatua tatizo lako kwa niaba yako.

## Ishi Kama Hauna Changamoto

Wakati wa changamoto sio wakati wa kudhoofika kwako! Usikubali changamoto iwe sehemu yako ya kurudi nyuma bali ifanye kuwa kama ngazi ikupelekayo juu zaidi. Wakati wa changamoto sio wakati wa kuanza kuvaa hovyo kama mtu asiyekuwa na akili timamu. Inawezekana kabisa ukawa kwenye changamoto kubwa na umeniga tai shingoni.

“Changamoto yako sio tangazo”

Usiishi kama vile ni wewe pekeyako upitiaye kwenye changamoto. Kumbuka kila mmoja anapita kwa wakati wake kwani changamoto ni kawaida ya mwanadamu na kinachomuokoa mwanadamu ni imani kwa Mungu pekee!

Neno la Mungu linasema “….japo utu wa nje unaonekana umechakaa lakini ndani tunafanywa upya.” Una wasiwasi gani mpendwa? kwa nini unajidhoofisha wewe mwenyewe? Muonekano mbovu haukusaidii chochote. Kuvaa magunia hakumfanyi Mungu akujibu maombi yako bali yeye huangalia imani iliyoko ndani yako. Kama haumuamini hakika utavaa magunia na kutembea kama mtu aliyepoteza matumaini na bado ukaendelea kuumia tu bila msaada wowote.

Kwa maelezo mengine ni kwamba unapokuwa unajidhoofisha ni kujiongezea maumivu juu ya maumivu. Unapoonesha unyonge wako mbele za watu ambao ni mashujaa unajipotezea heshima yako bure. Hakuna anayependa kuzidiwa ama kupitwa maishani. Kila mtu hutafuta mdhaifu wake ili asiwe mwisho kabisa lakini apate mtu wa kujilinganisha nae ili yeye aonekane ana ahueni. Je, uko tayari kufanywa wewe ndio wa mwisho? Mwenye hali ngumu zaidi?

Ukiishi hivyo; mbele ya wakuu hautasikilizwa na wala hakuna mtu atakayetaka kuwa karibu na wewe wala kuonekana kwamba anaambatana na wewe. Nyenyekea lakini huku ukiilinda heshima yako.

> Unapokuwa kwenye changamoto sio muda wa wewe kuanza kulaumu watu na kumuambia kila mmoja yale unayoyapitia. Kama sio lazima na hapana msaada wowote kwa unayetaka kumueleza jaribu kujizuia kabisa kuyaeleza matatizo yako mpendwa!

Ni ukosefu wa hekima endapo utakubali kujionesha kwamba wewe ni dhaifu kwani Mungu hakuweka hata chembe ya udhaifu kwako! Fungua macho yako na utazame! Wote wanaokuzunguka hapo ulipo wana matatizo tena pengine ni makubwa kuliko uliyonayo

wewe lakini wameamua kumuamini Mungu na wametulia kwa amani tele wakiwa na matarajio makubwa! Kinachokuumiza wewe ni ukosefu tu wa imani.

Kuna ndugu alinifuata na kunieleza shida zake na akawa anaamini kwamba anachopitia yeye ni kikubwa zaidi. Nikamsikiliza kwa dakika kama tano halafu nikamwambia na mimi napitia nini. Nilichokuwa napitia mimi kilikuwa ni kikubwa kuliko chake lakini tai ilikuwa haitoki shingoni na wala hakuweza kunikuta nimevaa kama mwehu. Basi akashangaa sana! Nikamueleza kwamba Mungu hakutupa roho za woga bali za nguvu. Nawe pia ujue ya kwamba hauna roho ya woga, aliyekupa woga huo mtafute umrudishie woga wake!

## Fikiria Maisha Bora Yajayo

Haijalishi tatizo lako ni gumu kiasi gani, bado haupaswi kupoteza taswira ya kesho yako iliyo bora! Hata kama adui kainuka na upanga, bado ona kesho yako ikiwa inakusubiria. Yohana akiwa kifungoni kwenye mateso katika kisiwa cha Patmo aliona mbingu mpya na nchi mpya vikishuka! Wewe unaona nini wakati wa changamoto yako?

Usikubali kuifikiria na uitamani jana yako kana kwamba ni bora zaidi! Wala usikubali kuona jana yako ni bora kuliko leo. Kama leo uko kwenye giza nene amini bado leo ni bora sana kuliko jana. Haupaswi kuithamini jana kuliko leo wala leo kuliko kesho! Maisha yako hayakujengwa kurudi nyuma bali kwenda mbele tu. Na mbele ni bora zaidi na zaidi na zaidi. Chukua hatua za kuisahau jana yako na ufikirie kesho yako kwa matumaini ya hali ya juu zaidi. Usiogope kuwa na ndoto kubwa, usiogope kujiwekea malengo makubwa!

Hali uliyonayo sasa isikushike, wala isikugandamize ni ya muda tu na haina madhara kwako bali inakujenga na kukufanya bora zaidi ili ufikie hizo ndoto zako zilizo kuu. Jaribu ni kawaida kabisa kwa mwanadamu! Usiiongee kesho yako vibaya na kuikosesha maana, usijipe mashaka na kesho yako amini tu! Maisha yetu yamefichwa kwenye imani na wewe ingia humo ili ufurahi.

> Yamkini ulikuwa na ndoto kubwa sana hapo awali lakini jaribu hili ulilonalo sasa linaweza kuwa ni giza nene sana na kwa kiasi fulani umeanza kusahau unapotaka kwenda na pale ambapo Mungu alikuonesha awali! Yamkini hauoni tena njia yoyote ya kutokea ili kesho yako

iwe bora! Ingia kwenye dimwi la imani potelea humo, hakika hautatahayarika!

Kwa kinywa chako unaweza kuiumba kesho yako na kwa ulimi wako unaweza kuikiri na kuikomboa kesho yako! Pale giza linapozidi inamaanisha kwamba kupambazuka kumekaribia. Umetenganishwa na giza tu hata usioone kesho yako lakini kumbuka giza likitoweka tu kesho yako itakuwa wazi sana hivyo hauna haja ya kuisahau kesho yako. Ifikirie, iboreshe, ifurahie na uikimbilie!

Ukweli utakuweka huru! Giza huja na kutoweka, na nuru ya Kristo huliutilia mbali giza lote. Wewe umtegemeaye Kristo usiwe na mashaka kuhusu kesho yako!

## Saidia Wengine Wanaopitia Changamoto

Moja kati ya mbinu kubwa za kisaikolojia za kuipa nguvu nafsi yako ni pamoja na kufanya mambo ambayo unaamini hauwezi kuyafanya. Unapokuwa hauna pesa za kutosha halafu ukamsaidia mtu mwingine asiyenacho kabisa, moja kwa moja utajiona una nguvu zaidi na wewe ni mwenye heri. Utaanza kupata nguvu na kuinuka kwa hatua moja moja mpaka utajikuta umefika mbali sana na tatizo lako litakutoka!

> Mwenye uhitaji ndiye husaidiwa, mwenye utoshelevu husaidia. Amini kwamba unao utoshelevu hata kama hauna utoshelevu huo kwa sasa. Msaidie anayepitia changamoto kama yako hakika wewe itakutoka! Unapomtoa mtu kwenye shimo na wewe shida zako hukuacha na kuingia kwenye shimo hilo ulilomtoa nduguyo kwa ukubwa huohuo. Ukisaidia kwa wingi zaidi ndivyo na wewe shida yako inakuondoka kwa wingi zaidi.

Wanadamu tumeumbwa ili tuishi kama jamii ama familia kwa lengo kuu la kusaidiana. Ukiwa nacho jitahidi kuhakikisha na mwenzio hajapungukiwa. Waswahili wanasema “kitamu kula na mwenzio” hata kama haujui kesho yako itakuwaje; usimnyime nduguyo chakula wala maji kama unayo. Jitahidi kuonekana kwamba wewe ni jawabu kwa matatizo ya watu na Mungu ataendelea kukujaza ili na wewe uwajaze wengine.

> Kuwa na changamoto sio kisingizio kukufanya usimsaidie mwenzio kwani changamoto ni kawaida ya mwanadamu. Likitoka hili litakuja na lile lakini usiache kumsaidia nduguyo akuitapo kama una uwezo huo.

Mungu amekufanya kuwa kiongozi katika jamii yako! Kiongozi hata akipitia magumu kiasi gani atahakikisha bado yeye anakuwa imara kuliko wengine na kutoitangaza shida yake kwa watu wake kama sio lazima. Tabia ya kiongozi ni kuvumilia magumu na maumivu yaliyomo ndani yake kwa namna yoyote. Watu wa kawaida kawaida huanza kuugulia maumivu na kupoteza uelekeo hata kutoka kwenye taarifa tu kabla hata jambo halisi halijamkuta!

Wakati mwingine tujiulize! Unapokuwa na familia halafu wewe ni baba au mama na unapitia jaribu, je, huwa unawaambia watoto wako wadogo? Kama hauwezi kuwaambia au kuwaonesha kwamba umekwama basi vivyo hivyo amini wewe ni kiongozi na kuna watu wanakutarajia uwatie moyo na sio wewe kuwa chanzo cha wao kukata tamaa. Unapogundua kwamba una wafuasi wengi basi muombe Mungu akupe hekima ya kuwaongoza na pia akuwezeshe kukaa kimya na kuvumilia.

Wakati mwingine utamkuta kiongozi wa kundi kubwa la watu akipata ugumu fulani tu anaanza kuwanyanyasa wanaomzunguka au anaowaongoza. Kwenye familia; kama ni baba anaanza kuwa mkali bila sababu yoyote kama ni mama anaibua kiburi kisicho cha lazima! Hizo ni

mbinu za ibilisi kulifanya jaribu lako likuangamize kabisa! Kataa hali hiyo na ishi kana kwamba haupitii changamoto ili uwe na amani tele ya kukuwezesha kuchukua hatua na maamuzi yaliyo bora hata wakati wa changamoto yako huku ukiamini kwamba Mungu anashughulikia swala lako.

# SURA YA TANO

## LIFANYE KOVU LAKO LIWE NA THAMANI

Katika maisha Mungu hutupa fursa mbalimbali za kujifunza ili kuyasogeza maisha yetu mbele ikiwemo kupita kwenye majaribu ambayo ni mtaji kwetu. Elimu yoyote unayoipata leo ni mtaji wako wa kesho ili kukupa maarifa na mbinu mbalimbali za kutatua matatizo yako binafsi, ya familia yako pamoja na matatizo ya jamii yako.

> Unapokuwa umepata fursa hiyo ni lazima uhakikishe umetoka na kitu cha thamani ndani yake! Unapoingia shimoni kutafuta madini unapofanikiwa kutoka hakikisha umebeba mali ambayo ni ya uhakika! Nakumbuka nilipokuwa nasoma chuo kikuu, nilihakikisha kwamba sifeli mtihani wowote hasa mtihani wa kumaliza muhula; na ndivyo ilivyokuwa kuanzia mwaka wa kwanza mpaka wa mwisho; kwa neema ya Mungu sikurudia mtihani wowote! Nilifaulu yote na tena kwa viwango vya juu!

Ninachomaanisha ni kwamba unapopata fursa usiiache ikapita na wewe ukabaki mtupu. Jaribu ni fursa! Unaweza

ukapita kwenye jaribu na likakuacha bila thamani yoyote usipokuwa makini. Na ukishindwa kulivuka litakuelemea na pale ambapo utakata tamaa ndipo hapo utajikuta maisha yako hayaendelei, utaishia hapohapo kwenye kiwango ambacho umeshindwa kukivuka. Yaani kama ikiwa ni shuleni na unafeli mtihani wa kidato cha nne utakisoma hicho kidato mpaka ufaulu ndipo utaona upenyo mpya ama la basi utaishia hapohapo mpaka uondoke duniani!

## Weka Malengo Yako Kwa Upya

Unapokuwa umepitia changamoto hakikisha kwamba changamoto yako inakuwezesha kuifanya kesho yako iwe bora zaidi. Zile ndoto zako ziwe halisi zaidi na maisha yako yawe kwenye uelekeo ambao Mungu anataka uendee. Wakati wa jaribu lako utakutana na mada tofauti tofauti za kujifunza na mahala pengine utagundua kwamba njia uliyokuwa ukiiona ni njema sio njema tena.

Kuna watu wengine huingia kwenye majaribu ili waweze kuziona kesho zao zilizo njema. Unaweza ukawa uliwategemea sana wanadamu na ukawekeza maisha yako kwao ukiamini ya kwamba watakuokoa siku ya tabu zako na ulipopitia tabu yako ukagundua ya kwamba hawana msaada wowote. Hapo tayari utakuwa

umejifunza kwamba mwanadamu sio wa kumtegemea na wanaweza wakabadilika muda wowote usioutarajia; hivyo ukabadili mpango wako na kuanza kumtegemea Mungu kwa asilimia zote.

> Jaribu halijaja kukuumiza, limekuja kukuboresha ili uifikie hatima yako kwa uzuri na ubora zaidi pia ili uendane na mapenzi ya Mungu mkuu aliyejuu na aliyekuumba wewe ili utimize kusudi lake lililo jema!

Chukua muda wako na uutumie kufanya tathmini ya mambo kadhaa ambayo unahisi unajifunza wakati unapitia ugumu fulani; nukuu mafunzo hayo halafu wianisha na malengo yako ya miaka mitano mpaka kumi ijayo. Utagundua kwamba Mungu anakufundisha jambo fulani ambalo ukilipuuza na muda wake ukifika na likadhihirika litakurudisha nyuma sana!

Unaweza ukapata nafasi leo ya kujifunza jambo dogo tu lakini usilipuuze kwa maana Mungu anataka uanze kulifanyia kazi kuanzia sasa ili uwe salama kwenye siku za usoni. Usihisi kwamba halikuhusu wala halitokei hivi karibuni bali lichukue tu na uliweke kwenye kumbukumbu zako. Kwa mfano; yawezekana ukashuhudia mtu anauliwa kutokana na dhambi ya udhulumaji na wewe kwa wakati huo usione kama

inakuhusu kumbe mbele yako kuna mtego kama huo na wewe hukujua kama utafikia hatua hiyo. Endapo ukiweka kichwani kwamba kumdhulumu mtu mali yake kunaweza kusababisha kifo basi hakika utakuwa salama na mtego huo utaukwepa.

"Jaribu likujiapo; fikiria zaidi kwenye malengo yako na kwa gharama yoyote usiyasahau hata kama jaribu lako limekutia giza na hauoni mbele tena"

Unapaswa kuwa mtu wa malengo makubwa. Usiishi bila malengo kabisa! Iruhusu akili yako kukupa picha ya miaka mitano ijayo ya maisha yako! Usipokuwa na malengo utayumba yumba sana barabarani na pia utakatishwa tamaa kwa wepesi maana jaribu ni kama giza lijalo mbele yako kukufanya uyasahau malengo yako; na pale giza liondokapo halafu wewe ukawa bado unayakumbuka na una shauku ya kuyafikia basi utaitwa heri. Yule ambaye ana malengo na jaribu lilipokuja likamfanya ajione hafai tena, akakata tamaa na kupoteza uelekeo, huyo ajitahidi kukumbuka ndoto yake na ahakikishe ile ari ya kufikia malengo imemrudia. Mbaya zaidi ni kwa yule ambaye hana malengo kabisa; hakika jaribu lijapo atapoteza uelekeo na kwenda kama upepo!

## Fanya Jaribu Lako Kuwa Ushuhuda

Duniani tunayo dhiki na tunapaswa tujipe moyo mchana na usiku. Katika kurasa zilizopita tumeona kwamba tunapaswa kujiweka karibu na watu wanaoifanya mioyo yetu iwe imara, wanaotutia nguvu, wanaotutia moyo na kutufariji. Kama wewe umepata mtu wa kukufariji basi na wewe fanyika kuwa faraja kwa wengine wote wanaokuzunguka! Usiwe kikwazo bali fanyika baraka. Hata kama bado Mungu hajakujibu ombi lako haimaanishi utumie nafasi hiyo kuwarudisha nyuma na wengine walio katika magumu.

Mungu kakupitisha hapo ili uweze kuwasaidia na wengine wanaopitia hapo! Katika kukua kwangu nimeshuhudia watu wanaojisifu kuwa walivuka salama na kuwakejeli wale ambao bado wameshikiliwa na magumu yao. Badala ya kuwapa mbinu, wao wanawashangaa na kufanya mashindano nao! Ni utovu wa nidhamu na ukosefu wa hekima kupambana na mtu ambaye yuko kwenye hatua ya chini yako. Wewe unapaswa kumsaidia uliyemzidi ili afike hapo ulipo wewe na sio kumcheka.

> Tatizo kubwa tulilo nalo ulimwenguni kwa sasa ni kwamba wanadamu wengi ni wanafiki. Kwa maneno atakueleza kwamba anataka kukusaidia lakini katika uhalisia hana mpango huo na hata akikusaidia hatapenda ufike katika hatua ambayo yeye ameifikia.

Kwa sababu hiyo tuna watu wengi sana wenye ndoto kubwa nazo zimezimwa na watu ambao waliwaamini na kuwaeleza mipango yao yote ili wapewe msaada; lakini kwa bahati mbaya walioelezwa wametumia taarifa hizo kama njia ya kuwaweka kwenye vifungo vya kimawazo na kuwafanya kuwa wategemezi ama vibaraka wao.

Inauma sana pale ambapo unategemewa ulete mabadiliko halafu unamfanya anayekutegemea umsaidie awe kibaraka wako! Hiyo ni dhambi na iko mbele yako. Kama unafanya hivyo; acha mara moja!

Unaua ndoto ya mtu endapo ukiweka ndani yake kitu ambacho sicho! Unashirikiana na shetani kwa asilimia zote na wala kwenda kanisani hakukusaidii na hakutakusaidia kabisa! Kumbuka dhambi yako itakurudia, hata kama sio kwako wewe itarudi kwa watoto wako endapo usipoitubia.

Kuna baadhi ya watu ili wakupe msaada wanataka uwalilie sana, uwanyenyekee kupita maelezo na ujioneshe kuwa ni mpuuzi; usiye na thamani mbele zao ndipo wakusaidie! Kwa kumfanya mtu awe hivyo hata ukimpa msaada hatakuwa tena na ari ya kusonga mbele na kuvuka vizuizi kwani atakuona wewe ndiye uliyeweza kufanikiwa, mwenye ufahamu mkubwa na hawezi kufanya zaidi yako kwenye jambo lolote! Msaada wako na wenyewe unakuwa ni upuuzi tu.

> Weka lengo leo la kutokushindana na watu kwani haujui ndani ya mtu Mungu ameweka nini, ukiwa mmoja wa watu wanaoua malengo ya watu, ni majuto na laana kubwa juu yako katika siku za usoni, inauma!!

Kitu chema ni kumfanya unayemsaidia ajisikie mwenye nguvu kabla haujampa msaada wowote na umuaminishe kwamba hata wewe umefika hapo kwa neema tu na yeye endapo akijipa moyo basi atafanya hata zaidi ya kile ulichoweza kukifanya; hapo msaada wako utazaa matunda na matunda ya huyo ndugu yatakuinua hata wewe na vizazi vyako katika siku za usoni.

## Kubali Kulipa Gharama

Jaribu ni njia ya kukufikisha mahala bora na panapovutia zaidi! Usipuuze maarifa uyapatayo katika jaribu lako. Wakati wa jaribu lako hakikisha unajengeka kwa namna tofauti tofauti kana kwamba hauko kwenye jaribu. Jipe muda wa kujifunza na kuweka kwenye vibao vya moyo wako mambo yote ya muhimu ambayo umejifunza. Mwanafunzi mwema hufaulu mitihani yake na hupewa tunzo mwisho wa mafunzo; cha muhimu zaidi ni kuwa na maarifa juu ya kile alichokuwa anakisomea ama kujifunza!

Changamoto ya kifenda inakutaka elimu yako ya kipesa iwe imara kwako ama iboreshwe ili ukifikia hatua nyingine uwe na maamuzi bora juu ya pesa inayopita mikononi mwako! Changamoto ya ndoa unakutaka uboreshe mahusiano yako. Utambue ni mambo gani mwenzi wako hayapendi. Utambue ukweli kuhusu mwenzi wako hata kama alikuficha baadhi ya mambo. Uwe baba au mama bora! Nakuhakikishia pale utakapokataa kulipa gharama na kujifunza, ukaamua kumuacha mkeo ama mumeo na kwenda kutafuta ndoa nyingine hakika changamoto ileile itajirudia! Ni sawa na mwanafunzi aliyefeli kidato cha nne na kumua kuhama

shule; bado atalazimika tu kukirudia kidato hicho mpaka pale atakapofaulu!

Kubali kujengwa na jaribu ili usirudie rudie somo hilohilo muda wote. Utachelewa! Wenzio hukubali kupitia changamoto na wanapata hatua nyingine ya kuendelea mbele ili wapate mafanikio makubwa zaidi kuliko yale ya awali ama yale waliyoyakuta kutoka kwa wazazi wao na wakarithishwa!

> Kwa mfano; mfanyakazi wa serikalini ama shirika lolote apandishwe cheo na kuongezewa mshahara yampasa aende shule akaongeze ufahamu wake juu ya swala husika ndipo arudi na apewe stahiki zake hizo!

"Endapo ukiamua kukwepa-kwepa changamoto, basi na maendeleo yako yatakukwepakwepa!"

Tunalo wimbi kubwa la watu wanaopenda kukwepakwepa changamoto ama majukumu yaliyo mbele yao na wao mafanikio ama maendeleo yanawakwepa-kwepa. Wanatafuta njia rahisi lakini wapi! Wakienda kulia wanaambiwa wameacha mafanikio yao kushoto; wakirudi kushoto wanaambiwa wameacha mafanikio yao kulia. Wanabaki wanahangaika kutafuta

mafanikio kwa Mungu mara kwa shetani lakini kote na mwisho wa siku wanakosa tumaini kabisa.

Ili uwe na amani; acha tabia ya kukinzana na uhalisia wako! Ili uwe bora na mwenye thamani usiogope kukabiliana na changamoto zako! Ukiwa bingwa wa kukinzana na mafuriko kwa kutumia mikono na kifua chako hakika yatakushinda nguvu na kukugharikisha kwani yapo kwenye mkondo wake na yanapaswa kupitia hapo hata kama wewe hautaki. Kubali kupitia changamoto, kwa amani tele mkabidhi Bwana ugumu unaopitia; hakika utavuka salama na ukiwa bora zaidi.

## Kifanyie Kazi Ulichojifunza

Umasikini na ujinga bado umejaa duniani kwa sababu tunao watu wengi wenye elimu kubwa na wengine wamezisomea katika maeneo maalumu yanayotoa elimu hizo kwa viwango vya juu duniani lakini tatizo kubwa ni kwamba hawafanyii kazi kitu walichojifunza. Haijalishi umesomea nini, haijalishi unajua nini lakini kama unajua kwa maneno tu hakika wewe na asiyejua ni kitu kimoja. Tena wakati mwingine asiyejua kabisa ni bora kuliko wewe; kwani wewe umetumia rasilimali vibaya. Umepata nafasi ya kujifunza lakini hatimaye umeishia kuwa kama chombo kisicholeta tija kwako binafsi, kwa

familia yako na hata kwa jamii. Halafu kwa bahati mbaya bado unadai ulipwe pesa ama mshahara kwa ujuzi wako ulio butu. Hiyo ni dhambi, uliaminika ukapewa nafasi lakini kumbe wewe sio mwaminifu!

> Unapopitia kwenye jaribu; ni furaha ya Mungu kuona umejengeka vema na unatendea kazi kile ulichojifunza ili uwe bora zaidi. Pale ushindapo jaribu lako usiwe kama debe tupu lipigalo makelele mengi pasipokuwa na kitu ndani yake. Ifanye furaha yako iwe ya kweli na yenye manufaa zaidi kwako na kwa jamii yako.

Kuwa wa tofauti na uhakikishe kwamba unachokifurahia baada ya kulishinda jaribu lako ni kwamba; uko tayari kupambana na adui aliyeko mbele yako na tena ukiwa umejawa na hamasa kubwa ya kumuendea na kumshinda. Hakika utakuwa mkuu siku zote!

# NUKUU BINAFSI

..................................................................

..................................................................

..................................................................

..................................................................

..................................................................

..................................................................

..................................................................

..................................................................

..................................................................

..................................................................

..................................................................

..................................................................

..................................................................

..................................................................

..................................................................

..................................................................

..................................................................

..................................................................

..................................................................

..................................................................

..................................................................

..................................................................

..................................................................

# NUKUU BINAFSI

.............................................................

.............................................................

.............................................................

.............................................................

.............................................................

.............................................................

.............................................................

.............................................................

.............................................................

.............................................................

.............................................................

.............................................................

.............................................................

.............................................................

.............................................................

.............................................................

.............................................................

.............................................................

.............................................................

.............................................................

.............................................................

.............................................................

.............................................................


## KITABU KINGINE CHA MWANDISHI

Kwa neema ya Mungu Aprili, 2017 Mwandishi Ezekiel Vigello aliweza kuzindua kitabu mahususi kwa ajili ya kuwatia moyo watu wenye ndoto ya kufanya biashara, wanaoanza kufanya biashara na wafanyabiashara wakomavu kinachoitwa;

**THE PATHS OF A TRADER**

tafsiri yake kwa kiswahili ni;

**MAPITO YA MFANYA BIASHARA**




**Jipatie Nakala yako sasa;**

**Barua pepe:** zekbanger@gmail.com

**Amazon: https://goo.gl/yEgmjs**

**Whatsapp:** +255 719 053 055

**Simu:** +255 753 100 788